

**22 SEPTEMBA, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 22 Septemba, 2022**

(Bunge Lilianza Saa Tatuhu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tilia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022*).

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022*).

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**22 SEPTEMBA, 2022**

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 114

**Ukarabti wa Kituo cha Afya Bungu – Korogwe**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya Bungu Wilayani Korogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Bungu ni kikongwe, chakavu na kipo kwenye eneo finyu. Serikali imefanya tathmini na kuweka mpango wa kujenga kwa awamu Kituo cha Afya kipya kwa gharama ya shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe katika mwaka wa fedha 2023/2024 itatenga kutoka mapato ya ndani shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Bungu. Aidha, Halmashauri itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo hicho. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kama alivyosema, kituo hiki ni kikongwe, hakuna ufinyu wa eneo. Kwa kuwa kutoka kituo hiki mpaka kituo kingine cha hadhi kama hii ni kilomita 50: Serikali haioni sasa ni vizuri kwa dharura ikawaonea huruma watu wa Bungu, angalau kuwajengea jengo la upasuaji au jengo la mama na mtoto ili kuwasaidia wananchi hasa akina mama na watoto? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wakati tukiwa tunasubiri hizo fedha na taratibu nyingine zote zikamilike, wananchi hawa wanateseka: Ni lini Serikali itapeleka gari la uhakika la wagonjwa ili kuwasaidia wananchi wa Bungu, kutoka Bungu kwenda mpaka Korogwe Mjini kilomita 50 kupata matibabu? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki cha Afya cha Bungu kiko katika eneo lenye ukubwa wa ekari mbili, lakini standards zetu za vituo vya afya ni angalau ekari kumi na Serikali imefanya tathmini kwa aina ya uchakavu mkubwa wa kituo kile cha afya, haitakuwa na tija kuweka fedha za kukarabati kituo kile. Ni vema kujenga kituo cha afya ambacho kitaendana na ramani za kisasa. Bahati nzuri kituo hicho kinajenga ndani ya Kijiji kile kile cha Bungu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo cha afya kitajenga katika kijiji kile na Halmashauri itaanza kutenga fedha katika mwaka ujao wa fedha mpaka kitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununua magari ya wagonjwa. Ni wahakikishie Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe pia itapelekewa gari la wagonjwa ndani ya mwezi ujao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa Ubungo, sasa aulize swali lake.

Na. 115

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Mabasi  
Yaendayo Kasi (DART)**

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO** aliuliza:-

Je, nini hatma ya wananchi wa Ubungo Kisiwani waliofanyiwa tathmini ya kulipwa fidia ili wapishe ujenzi wa mradi wa mabasi yaendayo kasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
(MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la makazi ya watu la Ubungo Kisiwani lilifanyiwa uthamini na kuandaa jedwali la uthamini lililotibitishwa na kusainiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali mwezi Aprili, 2022 lenye jumla ya Shilingi bilioni 7.87 zitakazolipwa kwa wananchi 90 wa eneo hilo watakaopisha ujenzi wa Karakana hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia hiyo kwa wananchi 90 na mara zinakapopatikana malipo hayo yatafanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mkumbo, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alifika katika Mtaa wa Ubungo Kisiwani tarehe 14 Mei, 2022 akafanya mukutano na wananchi pale na kulikuwa na mgogoro wa kiwango. Aliagiza kwamba wataalam wakafanye tena tathmini ili warudi kwa wananchi waelewani kuhusu kiwango ambacho kinastahili. Je, ni lini hiyo ripoti itapatikana?

Mheshimiwa Spika, la pili. Kwa kuwa muda mrefu umepita na wananchi pale hamna kinachofanyika na hata anuani za makazi hazijafanyika pale kwa sababu ya suala hili: Kwanini Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri msitoe tamko kwa sababu fidia hii haijulikani italipwa lini na wananchi wanaendelea na maisha yao kama kawaida? Ahsante. (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
(MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, Mthamini Mkuu alishamaliza kazi yake na alishasaini. Kwa hiyo, baada ya hili zoezi kukamilika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, ni kutafuta fedha. Kwa hiyo, kikubwa ni kwamba tutarudi kukaa na wananchi na kuwaeleza haya yote ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwondoe tu hofu Mheshimiwa Waziri kwamba kauli ya Serikali ni kwamba bado tunahitaji kuendelea kulitumia lile eneo, na ndiyo maana tunatafuta fedha ili tuwalipe kwa wakati. Kama muda utakuwa umepita, maana yake kuna options mbili kwenye sheria. Moja, kurudia uthamini; na pili, kunaweza kukawa na *interest* ili kuhakikisha kwamba wale wananchi wanapata fidia stahili kutokana na kutoa eneo lao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya ulipaji wa fidia inawakumba pia wakazi wa Mbagala, maeneo ya Kokoto mpaka Kongowe na Tuangoma, bado wanadai fidia kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya *Kilwa Road*; na kwa kuwa toka imefanyiwa tathmini mwaka 2019 mpaka leo hii hakuna malipo yoyote yanayofanyika kwao: Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia hiyo kwa wananchi wa Mbagala – Kokoto mpaka Kongowe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wote ambao wamefanyiwa tathmini yao watalipwa haki zao kwa sababu Serikali haina muda wa kutaka kwenda kumtapeli mwananchi yejote. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi huo. Kwa sababu Serikali ni moja, barabara ile najua iko upande wa *TANROADS*, basi tutafanya kazi hiyo kwa pamoja kuhakikisha jambo hili linawafikia. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 116

**Uwekezaji Katika Sekta ya Michezo kwa Timu za Wanawake**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawekeza katika Sekta ya Michezo hasa kwenye timu za wanawake ili kuibua vipaji kwa watoto?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elius Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwekeza katika kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Shilingi milioni 183.5 zimetengwa kama kianzio katika kutoa huduma kwa timu zetu za Taifa ikiwemo timu za wanawake na Shilingi bilioni 10 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya michezo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Timu za Taifa za wanawake ambapo kupitia uwekezaji huu, timu hizi zimeendelea kufanya vizuri katika ukanda wa CECAFA na COSAFA na umewezesha timu ya *Serengeti Girls* kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia nchini India. Ahsante. (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa ya kuuliza swali la nyongeza. Swali linasema: Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu mkakati wa muda mrefu wa kuendeleza vipaji vinavyopatikana kutokana na mashindano ya UMITASHUTA na UMISSETA?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janeth, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Janeth amependa kufahamu kauli ya Serikali kuhusu kuendeleza vipaji vya vijana wetu vinavyotokana na UMISSETA na UMITASHUMTA.

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara yetu kwanza tumshukuru tumshukuru Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, amehakikisha kwamba michezo hii imerudi na ametoa maelekezo kwa Serikali. Tunashirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Elimu, pamoja na Wizara yetu, kuhakikisha michezo hii

inaendelea, kwa kuwa michezo hii ndiyo inatupatia vipajji vyta vijana wetu wanaonzia huko chini kuingia timu za Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yetu inaendelea ku-review kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya UMISSETA na UMITASHUMTA ili michezo hii iwe endelevu. Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 117

### **Hitaji la Meli Mpya Ziwa Tanganyika**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka usafiri wa majini Ziwa Tanganyika?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi wa na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika bajeti ya mwaka huu wa 2022/2023 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa meli mbili mpya, chelezo na ukarabati wa meli za Mv Liemba na MT. Sangara ili kuboresha hali ya usafirishaji katika Ziwa Tanganyika. Kati ya meli zitakazojengwa, moja ni ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo na ya pili ni ya kubeba mabehewa na malori yenye uzito wa tani 3,000.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kuitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) inaendelea na mchakato wa ununuzi wa Wakandarasi wa kutekeleza miradi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami niulize maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu ya Serikali kwa hatua ya

awali ya kutenga fedha, lakini sote tunajua; kutenga ni jambo moja na kutekeleza mpaka ujenzi ukamilike na meli ianze kutumika ni jambo lingine: Nataka kujua ni lini ujenzi wa meli hizo utakamiliwa na kuanza kutumika kwenye Ziwa Tanganyika? (Makof)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Serikali imewekeza fedha kujenga Bandari ya Kasanga, Bandari ya Kabwe, Bandari ya Kipili, Bandari ya Kigoma pamoja na Karema, lakini hatuna usafiri wa uhakika wa Ziwa Tanganyika wa kubeba mizigo pamoja na mazao ambayo yanazalishwa kwenye hii mikoa mitatu. Nataka kujua kwa sababu huu muda ni mrefu wa kutengeneza hizo meli: Mna mpango wowote wa dharura wa kutuletea usafiri ili kupusha tatizo la kila siku kupoteza maisha ya Watanzania kwa sababu ya kutumia maboti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala usafiri ndani ya Ziwa Tanganyika. Nami nimeshuhudia nilikwenda kule, kuna changamoto kubwa hiyo. Nataka nimhakikishie Mbunge na Wabunge wote wa mikoa yote mitatu; Mkoa wa Rukwa, Katavi pamoja na Kigoma, suala la kukamilika, kwanza kama ambavyo nimesema kwenye jibu langu la msingi, tumeshatangaza tenda tarehe 19 ya mwezi huu wa Tisa, tunategemea zitafunguliwa tarehe 2 Novemba na tayari Mheshimiwa Waziri wangu, Profesa Mbarawa alishakwenda kule kuonesha hata sehemu ya kujenga chelezo kwa kampuni ambazo zimeonesha kwamba zina nia ya kwenda kutengeneza ama kujenga hizi meli mpya mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa swalii la pili, kwamba ni namna gani tunaweza kama Serikali tukafanya jambo la dharura kwa ajili ya wananchi wa mikoa hii yote mitatu; kwanza, tumejipanga katika kukarabati meli zote mbili. Kuna meli ya Liemba pamoja na Mv Mwongozo. Tenda ya Mv Liemba, inatangazwa tarehe 26 ya mwezi huu na tunategemea kwamba itachukua muda wa mwaka mmoja. Kwa Mv Mwongozo ambayo inabeba abiria 500 na tani 150 yenye kazi ndani ya Ziwa Tanganyika. (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swalii la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nililitaka kujua, ni lini meli ya MV. Kaliasi itaanza tena safari zake kutoka Bandari ya Mwanza, Kwenda Bandari ya Nansio Visiwani Ukerewe? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi wa Uchukuzi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna meli katika Ziwa Victoria ambayo ilipata shida katika mifumo yake ya kuongozea meli, na tulishaagiza kifaa hicho nje ya nchi; na ndani ya mwezi wa Kumi mwanzoni tunategemea kitakuja, kinaitwa *mouse controller*. Kwa hiyo, mwishoni mwa mwezi wa Kumi meli hii itaanza kufanya kazi zake ndani ya Ziwa Victoria. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Ally Makoa, Mbunge wa Kondoa, sasa aulize swali lake.

Na. 118

#### **Mwelekeo wa Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Handeni hadi Kwamtoro**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, kuna mpango wowote kubadili mwelekeo wa ujenzi Barabara ya Tanga kuitia Handeni, Kiberashi, Mrijo, Mondo Bicha hadi Kwamtoro?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya upembizi yakinifu na usanifu wa kina, ujenzi wa barabara inayounganisha Mikoa ya Tanga, Manyara, Dodoma na Singida utaanzia Handeni - Kibirashi - Kijungu - Kibaya - Goima - Chemba - Donsee – Kwamtoro hadi Kititimo (Singida) ambayo itakuwa na urefu wa kilometra 463.5.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii umeanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kujenga Kilometra 20 kwa sehemu ya Handeni – Mafuleta, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa wananchi wa Kondoa Mondo, walikuwa wanasubiria ujenzi wa barabara hiyo, sasa hivi inaonekana kwamba imekwepeshwa. Sasa Serikali ina mpango gani juu ya kuijenga barabara hiyo hiyo ambayo imeandikwa kwenye llani kutokea Mondo kwenda Kondoa - Bicha – Guseria kwenda kwa Mtoto?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, wananchi walikuwa na matumaini, kwamba kilomita hizi 400 zingepeita kwenye Daraja la Mto Bubu, je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuharakisha ujenzi wa lile daraja ambalo litaunganisha barabara hii iliyokuwa inategemewa ili kuondoa kero na kuokoa maisha ya wananchi na mali zao vinavyopotea kila mwaka ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Barabara ya kuanzia Goima – Mondo - Kondoa – Bicha, ipo kwenye llani na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri ya upatikanaji wa fedha barabara hii pia itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja katika Mto Bubu, Daraja la Mungwi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kondoa kwamba tunajua changamoto ambayo ipo, upembusi yakinifu wa daraja hili umeshakamilika na sasa hivi tutakamilisha usanifu wa kina. Meneja wa Mkoa ameshapewa kibali aandae pia na documents za kutangaza daraja hilo kuanza kujengwa. Kwa hiyo, litaanza kujengwa tu mara baada ya kukamilisha usanifu wa kina.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Bonifance Getere, swalii la nyongeza.

**MHE. MWITA B. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Ningependa kujua Barabara ya Bariri – Mgeta, ambayo ahadi yake ilitolewa na Mheshimiwa Rais, mwezi wa pili mwaka huu, ni lini itamaliza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Bunda – Mgeta kama alivyoisema, iliahidiwa na viongozi na sisi kama Wizara pamoja na Serikali tunaendelea

kutafuta fedha ili kutimiza hiyo ahadi ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Elinikiyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 119

**Ndege za Mizigo kutua bila Kulipa Landing Fees KIA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuufanya Uwanja wa KIA kutumika kuinua kilimo na kuruhusu ndege za mizigo kutua bila kulipa *Landing Fees*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikiyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna ndege mahsus za mizigo zenyet ratiba maalum zinazotua KIA. Mizigo yote inayopitia KIA hubebwa na ndege za abiria kwenye sehemu ya mizigo. Aidha, kwa sasa idadi ya ndege kubwa za abiria imeongezeka na hivyo kuongeza uwezo wa kubeba mizigo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya juhudhi mbalimbali kuimarisha biashara ya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya anga ikiwemo kununua ndege maalum ya mizigo (*Boeing 767 – 300F*) ambayo inatarajiwa kuingia nchini kufikia Juni, 2023, kwa lengo la kuhakikisha kwamba biashara hiyo inaimarika. Aidha, ili kuvutia biashara ya mizigo, Serikali ipo tayari kufanya mapitio ya *landing fee* kwa ndege za mizigo kama ilivyopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Serikali kwa kupokea ushauri na kuanza kuufanyia kazi, lakini naipongeza kwa kununua ndege za mizigo. Swali la kwanza; kwa kuwa sasa Serikali imekubali kupokea ushauri, je, Serikali iko tayari kutangaza Uwanja wa Kimataifa wa KIA kuwa uwanja wa kimkakati wa kusafirisha mazao ya kilimo na mifugo? (*Makofij*)

**22 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa tayari Serikali imeshatenga fedha na utaratibu wa kuanza kujenga common use facility ndani ya Jimbo la Hai. Je, Serikali haionti iko haja sasa ya kujenga kiwanda cha kutengeneza maboksi kwa ajili ya kusafirishia bidhaa zinazotokana na mifugo na kilimo? Pia kutanua cold room...

**SPIKA:** Umeshauliza maswali mawili Mheshimiwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Saasisha Elinikiyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili la ndege za mizigo. Katika maswali yake mawili ya kwanza anasema je, Serikali tuko tayari kutangaza uwanja huu kuwa ni wa kimkakati. Sisi Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri tunatangaza rasmi uwanja wa KIA kuwa ni uwanja wa kimkakati kwa mazao, hususan maua, matunda, mboga mboga pamoja na nyama pamoja na viwanja vingine kama cha Songwe International Airport kilichopo Mkoani Mbeya pamoja na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, anataka kufahamu ni kwa namna gani tunaweza tukashirikiana pia na wenzetu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika kukuza eneo hili na kujenga viwanda vidogo.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa KIA tayari tumeshatenga hekari ama hekta 711 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogovidogo, lakini pia kwa kushirikiana na wawekezaji na tayari tumeshaanza kufanya hiyo hatua. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Waziri.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Reuben Nhamainilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, swalii lake litalizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge.

Na. 120

**Hitaji la Umeme Mitaa 28 ya Jimbo la Handeni Mjini**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE K.n.y. MHE. REUBEN N. KWAGILWA**  
aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme mitaa 28 ya Jimbo la Handeni Mjini ambayo bado haijapata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Handeni Mjini lina jumla ya mitaa 60. Kati ya mitaa hiyo 32 ina umeme sawa na asilimia 53.3 na mitaa 28 haina umeme sawa asilimia 46.7.

Mheshimiwa Spika, Mitaa yote 28 ya Handeni Mjini ipo katika mpango wa kupatiwa umeme kupitia Mradi wa Umeme Vijiji, awamu ya tatu, mzunguko wa pili, unaoteklezwa na mkandarasi kampuni ya *Derm Electrics Tanzania* ambaye yupo eneo la kazi na anaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Handeni.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu utakamilika Mwezi Desemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoa na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini Serikali itajenga kituo cha kupozea umeme pale kwa Mbwembwele ili kuondosha tatizo la kukatikakatika katika Mji wa Handeni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mkandarasi anayesambaza umeme wa REA katika Wilaya ya Korogwe, anafanya kazi kwa kusuasua, tangu mkataba ulipoanza mwezi Mei, amesimamisha nguzo katika vijiji vitatu tu. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na mkandarasi huyu? (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Ulenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza Serikali tayari imetoa pesa, shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa grid ya Taifa na Wilaya ya Handeni ni mojawapo ya eneo ambapo patajengwa kituo cha kupooza umeme katika eneo la Mkata kwa kuanzia na kinajengwa mwaka huu wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili, mkandarasi anayepeleka umeme vijiji katika eneo la Korogwe, tutahakikisha kwamba kufikia Desemba mwaka huu anakamilisha kazi kwa sababu ndiyo mujibu wa mkataba. Tunaendelea pia kufuatilia kwa karibu kuondoa zile changamoto ndogo ndogo ambazo zilikuwa zimejitekeza za upungufu na ukosefu wa vifaa lakini kazi zitakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji 42 vilivyobakia katika Jimbo la Kalenga, Mkoani Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kupeleka umeme katika vitongoji vyote nchini kwa jinsi upatikanaji wa fedha unavyoendelea. Hatua ambayo tunaendelea nayo sasa ambayo inatakiwa kukamilika ni hatua ya vijiji ambayo itakamilika Desemba mwaka huu na fedha zinavyozidi kupatikana, vitongoji vinapelekewa pia umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme katika vijiji vya Kata ya Kiru na Magara, Jimbo la Babati Vijiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme vijiji katika eneo alilotaja utakamilika mwezi Desemba, Mkandarasi wa Giza Cable Industries Limited ambaye anapeleka umeme katika Mkoa wa Manyara, anaendelea na kazi na tutaendelea kusukumana naye ili akamilishe kazi kwa wakati.

**22 SEPTEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, mkandarasi anayepeleka umeme Kibaha Vijiji kwenye Kijiji cha Kimaramisale, tulikubaliana afike site kwa maelezo yake mwezi wa Sita na mpaka sasa hajafika. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa mkandarasi huyu ili akamalizie kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wote wa REA wako katika maeneo yao ya kazi mbalimbali. Unakuta mkandarasi mmoja katika mkoa mmoja labda ana wilaya nne au tano na tulipunguza kazi. Naomba nieleze kwamba baada ya hapa nitalifuatilia jambo hili kujua kwa nini mkandarasi huyu hajafika na kama amefika maeneo mengine basi ni lini atafika katika eneo la Mheshimiwa Mbunge alilouliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Kitongoji cha Ngana katika Wilaya ya Rungwe kina kaya 600, lakini waliowekewa umeme wa REA ni kaya 32 peke yake. Serikali haioni *interval* ni kubwa sana na ni lini itaweza kupeleka umeme katika eneo lile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maendeleo ni hatua na nia ya Serikali ni kuhakikisha kila mwananchi mahali popote alipo anafikiwa na umeme. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kupeleka umeme kwenye maeneo ya vijiji na vitongoji na kila mwananchi atafikiwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Erick James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

(Hapa Mhe. Erick Shigongo hakuwepo ili kuuliza swali Na. 121)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbongwe, sasa aulize swali lake.

Na. 122

**Askari wa Misitu Wanaopiga Wananchi – Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya askari wa misitu wanaopiga na kuwanyang'anya mkaa wananchi wa Mbogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Askari wa Uhifadhi wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, miongozo na maelekezo ya viongozi mbalimbali ikiwemo ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuzingatia haki za binadamu. Endapo kuna uvunjaji wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo, Wizara haitosita kuwachukulia hatua watumishi wake wanaohusika na uvunjaji huo wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na wimbi la uvunaji wa mazao ya misitu, ukataji na uchomaji wa mkaa bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia biashara hii. Hali hii imesababisha kutoweka kwa kasi kwa maeneo ya misitu na hatimaye kujitokeza kwa athari za mabadiliko ya tabia nchi. Hivyo, inapotokea mwananchi anasafirisha mazao ya misitu (mkaa) bila kufuata utaratibu, mazao hayo hutaifishwa na Serikali. Nitoe rai kwa wananchi wanaojishughulisha na biashara hiyo kufuata sheria, kanuni na taratibu husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; Mawaziri wale nane walikuja Mkoani Geita, kule Mbongwe kuna changamoto ya migogoro ya watu wenye uhifadhi, kuna Kijiji kimoja cha Sango, majuzi kimewekewa vizingi katikati ambapo kilishapata GN toka mwaka 1976. Je, Waziri, msimamo huu ukaje, maana wananchi mpaka sasa hivi wana hofu kulingana na kigingi kilichowekwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa amesema kumekuwa na wimbo la ukataji wa mkaa, lakini kuna utaratibu wa kisheria hawa wananchi huwa wanazifuata. Ila kuna hawa Askari Mgambo ambao pengine hawana mafunzo vizuri ya kusimamia hizi sheria; kumekuwa na mgongano pale wanapofanya hizi operation wanawakamata wananchi ambapo wanavibali tayari lakini wanaonekana kuwaumiza na kutowatendea haki. Je, ni nini kauli ya Mheshimiwa Waziri ili kusudi wananchi hao pale wanapofuata sheria zote wafanye shughuli zao vizuri? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mbunge wa Mbongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maeneo ya Mbongwe, baadhi ya vijiji vimeingizwa kwenye Kamati ya Mawaziri Nane na hivi ninayoongea tayari mikoa 13 imekwishatemebelewa na maelekezo ya Serikali ni kwamba tunafanya tathmini na wataalam wako katika mikoa hiyo 13 wanafanya hizi tathmini, lakini pia kuona sasa namna ya maeneo ambayo yamehalalishwa kumegwa, yamegwe kwa ajili ya kuachia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwa kuwa maeneo hayo yako ndani ya tathmini ambayo inasimamiwa na Kamati ya Mawaziri Nane wa kisekta, tutaendelea kutoa maelekezo kwamba wananchi wasibughudhiwe wakati tunasubiri majibu ya tathmini hiyo. Kwa hiyo, vizingi visiwafanye wananchi wasifanye shughuli zao za kila siku, na hao wahifadhi tunawaaelekeza wasilette vurugu yoyote mpaka pale ambapo tathmini ya Mawaziri nane itakapokamilisha kazi zake.

**SPIKA:** Hilo lilikuwa ni la kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya majibu ya swali la pili kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kwa hawa wananchi ambao wanakutana na changamoto ya kukabiliana na askari pamoja na wananchi. Niendelee kutoa rai kwa wananchi, kwamba tuendelee kufuata sheria, taratibu na kanuni zinazosimamia uvunaji wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na changamoto, tunatoa vibali tukiamini kwamba vibali hivi vitatumika ipasavyo, lakini tumekuwa na changamoto ya uanzishwaji wa usafirishaji wa mazao ya misitu kwa kutumia

pikipiki. Pikipiki inapita inaenda inavuna mti ambao haujaruhusiwa na wanapita njia zao za uchochoro, wakikamatwa wanasema wameonewa. Tuwaombe wafuate utaratibu na vibali vitolee kwa usahihi, ndivyo hawataktana na changamoto ya kukamatwana na mazao haya ya misitu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Licha ya kupewa vibali na sheria ilivyo lakini hawa askari, wakiwakamata watu hasa wenyewe baiskeli wanaobeba mkaa wanaharibu hata vyombo vyao vya usafiri. Je, Serikali inataka kutuambia kwamba sheria inaelekeza hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Askari wa Mazao ya Misitu wanapokuwa wanasimamia kwenye mageti, tuna changamoto kubwa sana ya usimamizi wa mazao haya. Ndani yake tuna askari wanaotoka kwenye halmashauri na kuna askari wanaotoka kwenye Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, kuna mkanganyiko hapa katikati ambao unajitokeza wakitaja maliasili, hata kama angekuwa ni Mgambo basi lawama inarudi Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, niendelee kuwaomba wananchi, kwa kuwa tuna vyombo vya dola; pale ambapo unatendewa vivyo sivyo ripoti na taratibu za kisheria ziweze kuchukuliwa haraka.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 123

### **Kutolewa Vibali vya Uwindaji**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, ni lini vibali vya uwindaji vitatolewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasli na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uwindaji wa wanyamaporu umegawanyika katika makundi mawili ambayo ni uwindaji wa kitalii na uwindaji wa wenyeji/wageni wakazi. Uwindaji wa kitalii ambao unalenga kupata nyara kwa ajili ya watalii unasihamiwa kwa kuzingatia Kanuni za Uwindaji wa Kitalii. Aidha, uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi hufanyika kwa ajili ya kitoweo na unasihamiwa kwa kuzingatia Kanuni za Uwindaji wa Wenyeji na Wageni Wakazi.

Mheshimiwa Spika, vibali vyaa uwindaji wa kitalii vinaendelea kutolewa kwa mujibu wa Kanuni husika ambapo hadi sasa jumla ya minada Saba imefanyika na wadau wamepewa vibali vyao. Kwa upande wa Uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi, vibali hivyo vitaanza kutolewa mara baada ya mapitio ya Kanuni za Uwindaji wa Wenyeji na Wageni Wakazi kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wengi hawa ambao walikuwa wanategemea kuuza nyamaporu walishajenga mabucha kwa ajili ya kuuza nyamaporu, kama ambavyo Serikali ilikuwa imewahamasisha. Mpaka sasa hivi vibali havijatolewa kwa muda mrefu na hasa kwa hawa wawindaji wa kawaida ambao wanalipa na leseni. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba hawa wafanyabiashara wa nyama ya pori wanapata hivyo vibali ili waweze kufungua mabucha yale ambayo walishayajenga?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hata pale nyama hiyo inapokuwa imepatikana kwa hao wachache ambao wanauzu, bei yake inakuwa ni ghali sana, na wananchi wengi wa kawaida wangependa kula hii nyama ya porini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mazingira mzuri kwa ajili ya kufanya hii nyama ya pori nayo iwe na bei ya kawaida ambapo kila mmoja anaweza kununua? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba tu niwatoe wasiwasi Watanzania na Mheshimiwa Mbunge kwamba vibali hivi vitatolewa baada ya mapitio ya Kanuni kukamilika. Tulikuwa na changamoto ya namna ya ugawaji wa vibali hivi kwa kuwa tuliweza kuanzisha makampuni ambayo tuliyakaribisha ili yaweze kuomba vibali vya uwindaji wa kienyeji. Lakini tumegundua changamoto inayojitokeza ni namna ambavyo tunaweza kuwanyima haki ya Kikatiba wananchi kuweza kupata kitoweo ambayo iko ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumepata maoni kutoka kwa wadau na sasa tumepitia Kanuni hizi, tunatarajia sasa kuzirejesha kwa maana tutoe ile haki ya wananchi, nao wawe na haki ya kuweza kupata kitoweo hiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya nyamapori, suala hili baada ya kuwa tumepitia Kanuni hizi na wananchi kuruhusiwa nao kuwinda uwindaji wa kienyeji, basi tunatarajia bei ya nyamapori kushuka kuliko ilivyo sasa ambapo tulikuwa tumependekeza makampuni pekee yaweze kuingia katika biashara hii. Ahsante.(Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda swali la nyongeza kwa kifupi. Mheshimiwa George Kakunda subiri kidogo, Waheshimiwa Wabunge, maswali ni mrefu mno na hakuna niliyemkatisha. Nawakumbusha kwamba maswali ya nyongeza yawe mafupi na majibu pia ya maswali hayo yawe mafupi. Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kuna malalamiko mengi sana ya wananchi kwa ajili ya kuruhusiwa uwindaji wa kienyeji, kwa nini Serikali sasa isiharakishe huo mchakato wa mapitio ya Kanuni usiku na mchana ili wiki ijayo waweze kutoa hicho kibali?(Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato umeshakamilika na hivi sasa uko kwenye *level* ya Waziri, wakati wowote tutaweza kutoa mapendelezo au maelekezo ya utekelezaji wake.(Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 124

**Mradi wa Maji Halmashauri 28**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Halmashauri 28 ambapo Njombe ni mojawapo utaanza kutekelezwa.?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa maji wa Miji 28 ambapo Wakandarasi wote walisharipoti site mwezi Julai, 2022. Kwa sasa, Wakandarasi wanaendelea na usanifu wa kina na ujenzi wa miradi kwa Miji 28 ikiwemo Njombe utaanza mwezi Novemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swalii la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunaishukuru Serikali kwa hatua hizo za awali. Ili mradi uweze kwenda na wakati ni lazima yale maeneo ambayo mabomba yanapita yaye wazi. Na ili yale maeneo ambayo mabomba yanapita yaye wazi, lazima wananchi walipwe fidia.

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao?

Swali langu la pili; je, ni lini mradi wa Igongwe wa Kata Nne za Jimbo la Njombe Mjini utapatiwa pesa ili Mkandarasi aendelee na kazi yake? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Mgaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninampongeza Mheshimiwa Neema kwa ufuatiliaji. Suala la fidia tunaelekea kulipa mradi unavyoendelea kujengwa na kila kitu kitakuwa kinakwenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, suala la mradi wa Igongwe kwenye Kata Nne, fedha zitaendelea kwenda kadiri tunavyozipata, na fedha ambazo zinifuata msimu ujao, huu mradi pia nao upo katika mpango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi wa Maji wa Izuga ni mradi wa muda mrefu, na kwa kuwa fedha iliyobaki ili mradi ukamilike ni milioni 76 tu. Kwa kuwa Mkandarasi yuko tayari walau apewe milioni 15 ili mradi ule ukamilike. Sasa, upo tayari baada ya Bunge hili mimi na wewe tuongozane mpaka Wizarani kuhakikisha kwamba Mkandarasi analipwa walau hiyo milioni 15 wananchi wapate maji? (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi atalipwa, nami niko tayari kwenda nawe site.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kupata mkandarasi wa maji kwa ajili ya mradi wa Kiwira ambao utalisha wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya. Sasa je, ni lini Serikali itatoa fedha ili mkandarasi aanze kufanya kazi mara moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali muhimu la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Suma kwa ufuatiliaji mzuri wa mradi huu muhimu ambao utakwenda kuleta manufaa kwa Mbeya Jiji na Wilaya jirani. Lini fedha inakwenda kupelekwa, tayari kazi zimeshaanza na Wizara tunafanya ununuzi na kupata Wakandarasi kwa

sababu Mhandisi Mshauri ameshakamilisha kazi yake. Hadi kufikia Desemba mwaka huu mradi utaendelea na utekelezaji. Kwa hiyo, kwa kila hatua fedha inatolewa. Fedha ilishaanza kutolewa toka Februari na sasa hivi ipo katika maandalizi ya kumpata Mkandarasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji uliopo Kata ya Mango Pacha Nne ili kuwatua ndoo kichwani akina mama hawa ambaa kwa muda mrefu, tokea tumepeata uhuru, hawajawahi kabisa kufurahia huduma hii ya maji safi na salama? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi utaendelea kuletewa fedha. Ninakupongeza Mheshimiwa Mbunge, ameshafuatilia sana huu mradi, fedha inakuja na mimi na wewe tutakwenda site kuhakikisha kazi inakamilika. Lengo ni kuona mwana mama anatua ndoo kichwani na ni dhamira safi ya Mheshimiwa Rais ambayo anayo kwa muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Serikali ilitenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa chujio la maji Wilayani Nyang'hwale kwenye bajeti ya 2022/2023 shilingi milioni 220.

Je, Serikali itatoa lini pesa hiyo na ujenzi uanze mara moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Hussein kwa sababu tulishafuatilia awali, mradi sasa umefikia hatua nzuri. Suala la chujio, hizi milioni 200 zitaletwa kwa wakati, mgao ujao pia tutapunguza hii fedha, angalau milioni 100 ili kazi ziendelee kufanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, utekelezaji wa agizo la Rais la kupeleka maji katika Kata Nne za Mererani, Endiamtu, Naisinyai, Shambarai na Oljoro Na. 5 umeanza katika Kata Mbili za Mererani na Indiamtu.

Je, ni lini sasa Wizara itatekeleza agizo hilo la Rais katika Kata zilizosalia kupitia Mradi ule Kabambe wa bilioni 400 wa Jiji la Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maagizo ya Mheshimiwa Rais kinachofuata ni utekelezaji, ndiyo maana katika Kata Nne tayari Mbili zimeshaanza kutekelezwa na Kata hizi Mbili pia lazima tuje tuzitekeleze ndani ya muda ambao Mheshimiwa Rais ametuagiza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kufahamu ni lini Serikali itapeleka maji Vijiji vya Kipingu na Kiogo ili kunusuru akina mama wanaoliwa sana na mamba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kamonga kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari tunao utaratibu wa kwenda kuhakikisha maeneo ya Kiogo na maeneo yote kandokando ya Ziwa yanapata huduma ya maji safi na salama bombani ili kunusuru wananchi ambao wanaliwa na mamba. Tayari nimeshamuagiza Meneja wa Mkoa wa Njombe na ameshaniahidi ndani ya muda mfupi atahakikisha eneo ambalo mradi ulikuwa haujafika unakwenda kukamilika. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa

kuniona, maana nimesimama muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mwaka wa Fedha uliopita tulikuwa na miradi mitatu mikubwa. Mradi wa Machiga, Mradi wa Chandama na Mradi wa Visima 13, lakini mpaka leo...

**SPIKA:** Uliza swali lako Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** ...mpaka leo Wakandarasi wote hawako site; naomba kujua kauli ya Serikali juu ya Wakandarasi hawa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Monni tumekuwa tukifanya kazi kwa pamoja na amefika Wizarani mara nyingi, nampongeza kwenye hilo. Miradi hii mikubwa ninaamini ameshaongea na Mheshimiwa Waziri, ameshaongea na Mheshimiwa Katibu Mkuu, tunakuja kutekeleza na Wakandarasi watafuata namna ambavyo wamesaini mikataba yao.(Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 125

**Kuanzisha Skimu ya Umwagiliaji Kata za Kaoze,  
Kipeta na Kilangawana – Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kujenga Skimu ya umwagiliaji Kata za Kaoze, Kipeta na Kilangawana kwa kutumia Mto Momba Kwela?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Vijiji kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kupima mabonde ya umwagiliaji yaliyopo katika Kata za Kaoze, Kipeta na Kilangawana ili kubaini eneo halisi linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, pia ulalo wa ardhi, kiasi cha maji kwa ajili ya umwagiliaji na aina ya mioundombinu itakayohitajika.

Mheshimiwa Spika, upimaji huo utahusisha hekta 16,000 katika Kata ya Kaoze, hekta 5,000 katika Bonde la Kata ya Kipeta na hekta 7,000 katika Bonde la Maleza, Kata ya Kilangawana. Kukamilika kwa upimaji huo kutawezesha maeneo hayo kuingizwa kwenye mpango wa uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 na kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu yenyewe matumaini kutoka Serikalini, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, utambuzi wa Bonde la Mititi na Ilembo ndani ya Jimbo la Kwela kwa ajili ya kuanzisha skimu umefanyika muda mrefu. Sasa nataka kujua, ni lini Serikali mtaleta fedha kwa ajili ya usanifu kuanzisha skimu hizo?

Swali la pili; skimu ya umwagiliaji iliyopo Kata ya Ilemba kwa maana ya Kijiji cha Sakalilo, imetumia muda mrefu sasa, imetumia zaidi ya Bilioni Moja, na bado fedha karibia Milioni 800 kukamilisha skimu hiyo. Nataka kujua ni lini wataleta fedha hiyo ili iweze kukamilisha skimu hii ya Sakalilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango hiyo tumeiweka katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 na imekuwa ni kilio cha Mheshimiwa Mbunge. Ahadi yetu ni kwamba tutafanya utekelezaji katika mwaka huu wa fedha na kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ni lini Mkandarasi wa kujenga Skimu ya Umwagiliaji ya Makwale Wilayani Kyela kutumia Mto Rufilio ataanza kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Jumbe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ambayo tuliyatoa kwa Wakandarasi wote wale ambao walisaini mikataba wakati wa sherehe ya Nanenane pale Mbeya ni kwamba wanapaswa kuwa site kuanzia tarehe 15. Lakini tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa hoja yake mahsus, basi tutahakikisha kwamba tunamharakisha Mkandarasi huyo aende kuanza kazi mapema kama ambavyo maelekezo yalitoka Wizarani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ardhi ambayo inafaa kwa umwagiliaji ambayo inatumika sasa hivi kwa miradi ya umwagiliaji ni pungufu ya asilimia Tano. Je, nini mkakati wa Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kuhakikisha maeneo yote ambayo yanafaa kwa umwagiliaji yanajengewa skimu? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali Na. 6 la Kitabu cha Bajeti cha Wizara ya Kilimo, imeelezwa mahsus kabisa kwamba Serikali imejipanga kuyafanyia upembuzi yakinifu na usanifu mabonde yote makubwa 22 ndani ya Nchi yetu ya Tanzania kuhakikisha yote yanafanya kilimo cha umwagiliaji, yakiwemo mabonde ya Mto Songwe, Ifakara, Idete, Pangani, Rufiji, Chamanzi na Malagarasi pamoja na Ziwa Victoria.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Naishukuru Serikali kwa kutoa fedha kuchimba bwawa la umwagiliaji katika Kata ya Chunyu, Namhambi: Je, ni lini kazi hii itaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa George Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi anayejenga mradi wa skimu ya umwagiliaji ya Msagali, hivi sasa yuko site ameanza mobilization na ni kati ya wale Wakandarasi 21 ambaao walisaini mikataba pale Nanenane Mbeya na tunategemea muda wowote aanze kazi hiyo. Vile vile bwawa ambalo linajengwa pale likikamilika litakuwa na uwezo wa kutoa lita za mita za ujazo milioni 92. Kwa hiyo, ni habari njema kwa wana-Mpwapwa na kwa bahati nzuri mkandarasi yuko site tayari. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swalii lake.

Na. 126

#### **Ripoti ya Ukaguzi ya Chama cha Msingi Nanjirinji 'A'**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, ni lini Ripoti ya Ukaguzi ya Chama cha Msingi Nanjirinji 'A' itatolewa ili hatua zichukuliwe kwa wahujumu wa fedha msimu wa 2021/2022?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Ukaguzi wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Nanjirinji 'A' ilikamilika Desemba, 2021 na kuwasilishwa kwenye Mkutano wa wanachama tarehe 23 Mei, 2022. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa udanganyifu katika nyaraka za mauzo ya ufuta na hivyo kusababisha malipo ya shilingi 93,476,190 kutolipwa kwa wakulima 89 waliouza kilo 39,319 za ufuta.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua ya kuvunja Bodi ya Chama hicho na taarifa ya uchunguzi imewasilishwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi kwa ajili ya uchunguzi zaidi na hatua za kisheria kwa waliohusika na ubadhifuru huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge swalii la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, shilingi 93,476,190 ni fedha za wakulima wangu wa ufuta 89: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakwenda kulipwa kwa wakulima hawa? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na changamoto zilizopo katika uendeshaji wa bodi zetu pamoja na vyama vyetu vyaa msingi na changamoto wanazozipata wakulima kwa uongozi usiokuwa madhubuti, Waziri atakuwa tayari kuambatana nami baada ya Bunge hili kwenda Nanjirinji kuzungumza na wakulima? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza la kuhusu malipo kwa wakulima, namwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushirika Tanzania kuhakikisha anafuatilia na mwisho wa siku wakulima hawa waweze kulipwa madai yao haya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu kuongozana na Mheshimiwa Mbunge, nimwahidi kwamba niko tayari, baada ya vikao hivi vyaa Bunge tuongozane mimi na yeze kwenda Kilwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan Mbunge wa Chakechake, sasa aulize swalii lake.

Na. 127

#### **Hitaji la Kituo cha Polisi Wilaya ya Chakechake**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kituo kipyaa cha Polisi katika Wilaya ya Chakechake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge Wa Chakechake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi lina eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Shehia ya Vitongoji lenye ukubwa wa mita za mraba 1,496. Mpango wa Serikali ni kutenga fedha katika bajeti ya mwaka ujao 2023/2024 ili ujenzi uanze. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ingawa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri kwenye swali lake la msingi, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba, wakati tunasubiri fedha zitengwe kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo kikubwa.

Je, Serikali haioni haja ya kujenga vituo vidogo vya Polisi (*Police Post*) kwenye maeneo tofauti ya Mji wa Chakechake? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufuatana nami twende kwenye eneo la Chakechake akaone jiografia na kama ujenzi wa Kituo cha Vitongoji ndiyo ingekuwa suluhisho la wananchi kufuata huduma za kipolisi? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni kweli kwamba pale ambapo pana umuhimu Serikali inaweza ikasaidiana na wananchi kujenga Police Post kwa maana ya vituo vidogo vya Polisi panapohitajika. Hata hivyo, kwa sababu Kituo cha Chakechake kwa sasa kimechakaa, kinahitajika kujengwa kituo kipyta, kipaumbele tumeweka kwenye kujenga kituo kipyta katika mwaka wa fedha ujao. Namwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane nasi tulitekeleze hilo kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili juu ya umuhimu wa kuongozana naye kwenda vitongojini, niko tayari, hakuna kikwazo chochote. Wakati utakapofika tukaambiana basi tutaongozana. Nashukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali dogo la nyongeza. Kama ilivyo Jimbo la Chakechake kuhusu kujengewa kituo; nami nimekuwa nikiuliza sana katika Jimbo langu la Chumbuni; na nimekuwa nikipewa ahadi zaidi ya mara sita, saba kwa vituo vyangu viwili vya Marubi na Chumbuni kuwa nitapata msaada kutoka Jeshi la Polisi na kujengewa; na tuliwahi kuuliza ikiwa Serikali iko tayari kuvirasimisha kwetu, kwa wananchi wa Jimbo la Chumbuni? Basi wafanye hivyo, halafu watupe kibali, nasi tunaweza kuendelea wenyewe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pondeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli amekuwa akiuliza maswali ya Chumbuni na nilimwahidi katika kipindi cha bajeti cha Aprili – Juni. Niliweza kwenda Zanzibar na nilitembelea kituo chake. Kinachogomba ni upatikanaji wa fedha ndiyo maana tunaweka vipaumbele. Mheshimiwa Mbunge avumilie na akubaliane nami kwamba pale tutakapopata fedha, Chumbuni itapewa kipaumbele kama tunavyofanya kwenye maeneo mengine ya Chakechake na kwingineko. Nashukuru. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale ina umri wa miaka 47 sasa, haijawahi kuwa na jengo la Kituo cha Polisi ukiacha lile jengo ambao wamepanga lililokuwa la benki. Nini, kauli ya Serikali kuipatia Wilaya ya Liwale jengo la Polisi? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Wilaya kongwe hizi zimekuwa na vituo lakini chakavu sana. Sasa kwa bahati mbaya Liwale hajawahi kuna nacho. Namwahidi kwamba katika bajeti ijayo tutaweka kipaumbele ili Wilaya yake ianze mchakato wa kujenga kituo chake cha Polisi kama zilivyo Wilaya nyingine za Tanzania Bara. Nashukuru. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nimwulize swali moja dogo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kituo cha Wete ndiyo Makao Makuu ya Polisi Mkoo wa Kaskazini Pemba. Kituo kimechakaa, hakina hadhi: Ni lini Serikali itakikarabati kituo kile? Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba vituo vingi vilivyojengwa siku nyingi vimechakaa sana. Kama atafuatilia, tumeanza kukarabati vituo vya Polisi vikianzia Makao Makuu pale Zanzibar na makazi yao. Tutaendelea kufanya hivyo maeneo ya Pemba kutegemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tumeshakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba awamu ijayo nitatembelea Pemba na eneo la Wete ni eneo nitakalolipa kipaumbele katika ziara yangu. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Omar swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu lilikuwa linalekeana na la Mheshimiwa Khalifa. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Issa swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Bunge liliopita la bajeti, Wizara ya Mambo ya Ndani iliniahidi kituo cha Konde kutengenezwa kwa thamani ya shilingi 41,500,000 na bajeti tayari tumeshapitisha.

Je, ni lini Wakandarasi watafika kwenye Kituo cha Konde na kuanza matengenezo? Ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Konde, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maadamu bajeti imepitishwa na ipo na anachosubiri ni Mkandarasi, tutawasiliana na Kamishna wa Polisi Zanzibar ili mipango ya kumpa Mkandarasi, kwa sababu tunatumia force account,

aweze kuelekezwa engineer wa Polisi Zanzibar ili ukarabati wa jengo hilo uweze kuanza. Nashukuru. (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 128

### **Mahakama kutoa hukumu ya Pande Mbili**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Mahakama kutoa hukumu ya pande mbili hasa mtuhumiwa anaposhinda kesi kuepuka usumbufu kufungua kesi mpya ya kulipwa fidia?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni na taratibu za madai ya fidia, kuachiwa huru kwa mshtakiwa katika shitaka la jinai hakumpi haki ya moja kwa moja ya kulipwa fidia. Ili mshtakiwa aweze kulipwa fidia kutokana na kushinda shauri la jinai, ni lazima athibitishe Mahakamani kwamba mashitaka dhidi yake yalikuwa ya hila; na kwamba hakukuwa na sababu za misingi za kumshtaki. Kuachiwa pekee kwa mshtakiwa katika shitaka la jinai hakumaanishi mashtaka dhidi yake yalikuwa ya hila na waliomshitaki hawakuwa na sababu ya kuamini alitenda kosa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 345(2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinaipa mamlaka Mahakama kutoa amri ya mtuhumiwa aliyeshinda shauri lake la jinai kulipwa gharama za shauri iwapo shauri hilo liliendeshwa na Mwendesha Mashtaka wa Kujitegemea (*Private Prosecutor*).

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mchakato uliopo unapoteza haki ya watu wengi kwa kutokupata haki zao kwa wakati, lakini wakati mwingine kwa watu wengine kushindwa kurudi

Mahakamani kwa hofu na woga: Je, ni lini Serikali itakuja na sheria ambayo inatoa haki kwa wakati huo huo wa hukumu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia swalii la pili; kumekuwa na utaratibu kwa watu kufunguliwa kesi baadaye kesi hizo zinafutwa, anafunguliwa kesi nyingine mbadala; je, ni vigezo gani vinatumika kumbadilishia mtu kesi kutoka ile kesi ya awali kuja kesi ya pili? Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kufanya marekebisho madogo ya sheria kwenye eneo hili tunalichukua na tunakwenda kulifanyia mchakato ili tuone kama kuna sababu zozote za kufanya hivyo na Bunge lako Tukufu litajulishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya kesi wakati umeshitakiwa kwa kosa hili na baadaye unapelekwa kwenye kosa lingine, hilo linategemea sana mwenendo wa upelelezi ambao unaweza ukabaini uhusiano wa tukio lile na tukio lingine ambalo linakupeleka kwenye mashtaka mapya. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa sasa aulize swalii lake.

Na. 129

### **Kesi za kodi kutoamriwa kwa wakati**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, ni nini kinachosababisha kesi 1,097 za kodi za muda mrefu zenye thamani ya shilingi trilioni 360 na dola za Marekani milioni 181.4 kutoamuliwa hadi sasa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Ahmad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi Agosti, 2022 kulikuwa na idadi ya mashauri 854 kwenye hatua mbalimbali za usikilizaji yenye kodi inayobishaniwa ya jumla ya Shilingi trilioni 4.21 na dola za Marekani milioni 3.48 katika Taasisi za Rufani za Kodi ambazo ni *TRAB* na *TRAT*. Hivyo, kwa sasa *TRAB* na *TRAT* zinaendelea kusikiliza mashauri hayo pamoja na mashauri mapya yanayoendelea kusajiliwa. Aidha, kwa nyakati tofauti idadi ya mashauri ya kodi hupungua au kuongezeka kulingana na kasi ya usikilizaji na usajili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika kwamba swali limeuliza shilingi trilioni 360 lakini limejibowi shilingi trilioni 4.21. Hata hivyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

La kwanza, kwa nini Serikali iliamua kukubali kupokea shilingi bilioni 700 kutoka katika kesi za malimbikizo ya makampuni ya madini maarufu "makinikia" badala ya shilingi trilioni 360 ambayo ni madai halali katika nchi yetu? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nini kilichowafanya *TRA* washindwe kukusanya malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi ya shilingi trilioni 7.54 na kusababisha ongezeko hili la malimbikizo ya kodi kufikia asilimia 94.6 lakini wakati huo huo uwezo wa *TRA* wa kukusanya malimbikizo hayo umekuwa ukishuka kila wakati na kufikia asilimia 10 tu na wakati huo *TRA* ikijivuna kwamba inaongeza makusanyo ya kodi?

Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kwanza nipate ufanuzi; swali linazungumzia kesi 1,097; shilingi trilioni 360 na hizo Dola za Kimarekani milioni 181.4.

Mheshimiwa Naibu Waziri jibu linazungumzia mashauri kuwa 854 ambayo thamani yake ni shilingi trilioni 4.21 na dola za Kimarekani milioni 3.48. Haya ndiyo mashauri yaliyopo ambayo Serikali inayajua ambayo ni tofauti na ya Mbunge au mmechagua kati ya yale ambayo yapo, mmeamua kuyajibia haya ambayo mmeleta majibu? Nataka kuelewa kwanza hapa. (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hayo ni mashauri ambayo yapo na Serikali tunayatambua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naona umesimama. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ufanuzi wa hiyo sehemu ya kwanza, halafu nimpe fursa ya kujibu yale maswali mawili.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwenye suala la msingi lile la shilingi trilioni 360; moja, Serikali haijakubali tu kimya kimya, haijakubali kupokea fedha hizo kwa maana ya kuacha shilingi trilioni 360, isipokuwa kilichofanyika, utakumbuka Serikali ilipeleka *complain against* makampuni hayo ya madini na baada ya *complains* zile kupelekwa...

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa, twende kwa mtiririko mzuri. Ninachotaka kuelewa, swali la Mheshimiwa Mpina linazungumzia kesi 1,097; jibu linazungumzia kesi 854 na thamani ambayo Mheshimiwa Mpina anazungumzia ni shilingi trilioni 360, serikali inasema ni shilingi trilioni 4.21. Mimi nataka kuelewa ili nitoe mwongozo vizuri wa majibu hapa, namna Serikali ijibu. Haya majibu ambayo Serikali mmetoa, ni kwamba ndiyo kesi zilizopo ama idadi ni hii aliyotaja Mheshimiwa Mpina na kiasi cha fedha ni hiki alichotaja Mheshimiwa Mpina?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, pana utofauti. Ile kesi kubwa aliyiongelea ya Shilingi trilioni 360 ni ya upande wa makinikia. Hii ya mashauri ambayo yanaenda kwenye shilingi trilioni nne, ni ya mashauri ya kesi nyingine ambazo ziko TRAB na TRAT ambazo ndiyo Serikali inaendelea kuyafanyia kazi moja baada ya nyingine.

Kwa hiyo, pana mambo ya aina mbili na lingine limeongezeka ya yale yasiyo ya kesi na lile linakuwa la tatu. Kwa hiyo yameunganishwa pamoja.

**SPIKA:** Sawa, sasa ili twende vizuri kwa sababu swali la Mheshimiwa Mpina lilikuwa mahususi linauliza hivi je, ni kwa nini kesi 1,097 za kodi zenye thamani ya shilingi trilioni 360 na dola za Marekani milioni 181.4 hazijaamuliwa mpaka sasa? ndio swali lake.

Jibu la Serikali linazungumzia mashauri 854 na thamani trilioni 4.21 na pia dola za Kimarekani zinazotajwa hapa ni tofauti na alizozuliza Mheshimiwa Mpina. Kwa hiyo ngoja nitoe fursa. Natoa fursa hili swali likajibewe yeze Mpina anavyotaka majibu yaani mjibuni kwa hizo bilioni na trilioni aliyoyasema. Kama yeze hayuko sahihi, ndio swali langu lilikuwa hapo, ili nielekeze vizuri hapa mbele, lakini kama unasema alichokiliza kipo, basi mjibuni majibu yake anayoyataka, kwa sababu haya majibu siyo ya swali lake. (Makof)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni, Mheshimiwa Waziri labda sasa atakuwa ameelewa tofauti.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, trilioni 360 haziko kwenye TRAB na TRAT ni kitu tofauti kabisa.

**SPIKA:** Hazipo kwenye nini?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwenye TRAB na TRAT.

**SPIKA:** Ndio nini?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, hazipo kwenye...

**SPIKA:** Hazipo kwenye nini? Mimi sielewi, maana yake nini?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, trilioni 360 hazipo kwenye mashauri haya ya kikodi ya TRAB na TRAT, kwa hiyo...

**SPIKA:** Sawa Mheshimiwa Waziri mimi nime...

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hayako kwenye rufaa za kikodi wala haziko kwenye *tribunal* ya kikodi. Hii ni jambo mahususi ambalo lilikuwepo kwenye mzozo wa Serikali pamoja na Barrick, kwa hiyo ni kitu tofauti, lakini kwenye nyongeza ndio ameuliza kuhusu masuala ya kesi sasa hizo ambazo ziko kwenye rufaa pamoja na *tribunal* ya kesi.

**SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Waziri nimekuelewa, kwa sababu yeye aliuliza swali tofauti ambalo ndio unalitolea majibu hapa. Sasa hayo majibu yaje yajibiwe kwenye swali lake kwa sababu ndicho alichouliza, kama hakipo ajibiwe hakipo na kama kipo usimledee kingine kwa sababu sicho alichouliza, ndio hoja iliyopo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri nakuruhusu ukakae. Hili swali kama liliyoulizwa na Mheshimiwa kwenye swali lake la msingi, liletwe majibu kama ndivyo liliyvo, halipo jibu halipo, si mnajibu kifupi siku hizi ndio raha yake, kama halipo halipo, kama lipo mjibuni yeye alichouliza kwa sababu ninyi mmemjibu kitu tofauti na ndio maana hata takwimu zinatofautiana. Ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ninyi mleteeni majibu kwa kadri alivyouliza swali lake, kama halipo jibuni halipo halafu yeye atapewa nafasi ya kuuliza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kwa sababu hapa nazungumza mimi na huwezi wewe ukawa unanipa mimi taarifa kikanuni, kwa sababu mimi ndio nazungumza, kwa hiyo ukiwa unanipa taarifa maana yake unaniongezea mimi jambo ambalo haliruhusivi kikanuni.

Mheshimiwa Naibu Waziri jibu hili itabidi lijibiwe upya pamoja na ufanuzi ambao ameutoa Mheshimiwa Waziri hapa ambao ndio unatakiwa uje kama majibu ya msingi.

Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Mlalo sasa aulize swali lake.

Na. 130

### **Kutumika Sheria ya Manunuzi na Ukandarasi Kupitia PPP**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Sheria ya Manunuzi na Ukandarasi kupitia *Public Private Partnership* itaanza kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ipo na inatumika, sambamba na Sheria ya PPP, Sura 210, ambapo mchakato wa zabuni za miradi ya PPP unazingatia sheria zote mbili. Pamoja na sheria hizo kutumika kama rejea wakati wa ununuza wa miradi ya ubia, Serikali inaendelea na utaratibu wa kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau ili kurekebisha vifungu vyenye changamoto katika utekelezaji wake. Ni matarajio yetu kwamba, marekebisho ya sheria zote mbili yatakamilika katika mwaka 2022/2023. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria hii ya PPP kwa maana ya Sheria Sura namba 210, kiwango cha mtaji kwa wazawa ni dola

milioni 20. Je, Serikali haioni kwamba kiwango hiki ni sehemu ya kikwazo cha utekelezaji wa sheria hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani wa kupunguza masharti ya kimkataba katika miradi hii inayoibuliwa na sekta binafsi ili iweze kutekelezwa kwa ufanisi kupidia *PPP*? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *PPP* ipo katika mchakato wa kufanyiwa marekebisho na sasa ipo ngazi ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira mpaka mchakato huo utakapokamilika bila shaka hiki hakitokuwa kikwazo kwa utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, masharti hayo ambayo yapo pia ni kwa mujibu wa sheria na taratibu, kwa hiyo pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge masharti hayo huenda yakapungua baada ya kupata mapendeleko kutoka kwa wataalam wetu ambao wanakusanya maoni hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 131

### **Elimu ya Sekondari Kuwa ya Lazima**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaifanya elimu ya sekondari kuwa ya lazima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa lengo la kuiboresha elimu yetu ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa na baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ipo katika hatua ya kupokea na kuchambua maoni ya wadau kuhusu Sera ya Elimu, hivyo suala la elimu ya sekondari kuwa ya lazima itategemea maoni ya wadau na mahitaji ya wakati. Rasimu ya kwanza ya Sera ya Elimu inatarajiwaa kukamilika mwezi Disemba, 2022. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, kwa kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha nia na dhamira ya dhati ya kumlinda mtoto wa kike, kwa kuweka elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita. Kwa nini sasa Wizara isitoe waraka wa kulinda watoto hawa dhidi ya mimba za utotoni na ndoa za utotoni ili kuwahimiza kuwa shuleni wakati tunasubiri mabadiliko makubwa ya sera?

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na wimbi kubwa la watoto mtaani...

**SPIKA:** Hilo ni la pili Mheshimiwa, la kwanza umeshataoa maelezo tayari, uliza swali lako la pili.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isitoe kauli dhidi ya watoto walioko mtaani wanaokosa kwenda shuleni ambao wamejiingiza kwenye makundi ya vilevi na uhalifu kama panya road? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba sasa Serikali tunafanya mapitio ya Sera pamoja na Sheria yetu ya Elimu. Nimeeleza hapa kwamba rasimu hiyo itakuwa tayari mwezi wa Desemba, 2022. Hata hivyo, uandaaji wa miongozo anayozungumza Mheshimiwa Mbunge pamoja na nyaraka mbalimbali zinategemea vilevile

mwongozo kutoka kwenye sera hii. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, kwa vile Desemba sio mbali tutakamilisha rasimu hii na huenda hayo yote anayoyazungumza yakawemo kwenye sera pamoja na sheria yetu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili mwaka jana, 2021, Serikali ilishatoa Waraka Na.2 wa Elimu wa mwaka 2021 ambao unahusu namna gani wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwemo na hii ya ujauzito wanaweza kurudi shulenii. Kwa hiyo tutoe wito tu na rai kwa wadau pamoja na mamlaka mbalimbali zinazosimamia elimu kuhakikisha kwamba tunakwenda kutekeleza maagizo haya ya Serikali. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 132

**Wahitimu Wangapi wa Kada ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hesabu Hawajajiriwa tangu Mwaka 2015**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, kwa takwimu ni wahitimu wangapi wa kada ya Ualimu wa masomo ya sayansi na hesabu hawajajiriwa tangu mwaka 2015?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2015 hadi 2022 jumla ya wahitimu 33,492 wa kada ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati wamehitimu mafunzo katika Vyuo mbalimbali vyta Ualimu na Vyuo Vikuu. Kati yao wahitimu 13,383 wameajiriwa katika shule mbalimbali nchini tangu mwaka 2015. Aidha, wahitimu 20,109 hawajajiriwa katika shule za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuajiri ili kukidhi mahitaji ya Walimu katika shule za umma. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Dunia ya sasa ni ya sayansi na teknolojia, hivyo kama Taifa lazima tuwekeze kuhakikisha kwamba tunakuwa na Walimu wa kutosha kwenye masomo haya ya sayansi na hesabu; na kwa kuwa kuna uhaba mkubwa sana wa Walimu waliopo ni takribani asilimia 33 tu. Je, ni nini mkakati madhubuti na wa haraka wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inaa jiri Walimu wa kutosha ili kukabiliana na changamoto hii?

Mheshimiwa Spika, swalı langu la pili; kwa kuwa wahitimu hawa ambao hawajaajiriwa tangu mwaka 2015 ni takribani asilimia 60 na wengi wao wamekuwa wakijitolea kufundisha bila ajira rasmi. Ni kwa nini Serikali isiwape kipaumbele Walimu hawa wanaojitolea kwa kuwaajiri kwenye maeneo ambayo wanajitolea kwa sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Matiko kwa ufatiliaji wa karibu wa Walimu wetu wa masomo ya sayansi pamoja na hisabati. Hata hivyo, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Serikali imeendelea kutoa fursa za ajira kwa Walimu hawa, tunajua changamoto ipo na uhitaji upo ni mkubwa. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI yenye dhamana ya kuomba vibali tayari katika mwaka huu wa fedha imeshaomba kibali cha kuajiri Walimu zaidi ya 42,697 ambapo kipaumbele kikubwa sana tutawapa Walimu wa sayansi pamoja na hisabati na wale ambao wanajitolea katika maeneo mbalimbali nchini. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 133

### **Kauli juu ya Wananchi Kuvunjiwa Nyumba – Tunduma**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Kata ya Majengo Tunduma waliovunjiwa nyumba zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 133 liloulizwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kabla sijajibu swali nitoe maelezo machache ya utangulizi. Kikao cha Makatibu Wakuu wa Nchi za Tanzania na Zambia kilichofanyika mwezi Oktoba, 2013, pamoja na mambo mengine kiliuzimia kwamba alama za katikati ya mpaka (*Intermediate Boundary Pillars*) kwa sehemu ya mpaka yenye urefu wa kilomita 50 ziongezwe ili kuzuia ongezeko la shughuli za kibinadamu na pia eneo la hifadhi ya mpaka lipunguzwe kutoka mita 100 kila upande zilizokuwa zinatambulika hapo awali hadi mita 50 kila upande. Hata hivyo, pamoja na maazimio hayo kutekelezwa, baadhi ya wananchi waliendelea kuvamia eneo la hifadhi ya mpaka kwa kujenga makazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017, Serikali ilitoa tamko la kuvunja nyumba zote zilizojengwa katika eneo la hifadhi ya mpaka suala ambalo lilipingwa na wananchi 134 kwa kufungua Shauri Na. 195/2017 katika Mahakama Kuu, Mbeya. Shauri hilo lilifutwa mwaka 2019 na hatimaye jumla ya nyumba 193 zilizokuwa ndani ya eneo la mita 50 za hifadhi ya mpaka zilibomolewa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo, wananchi 35 walifungua tena shauri Na. 12/2019 katika Mahakama Kuu Mbeya kudai fidia kutokana na kubomolewa kwa nyumba zao. Baada ya mazungumzo nje ya Mahakama (*mediation*) yenye lengo la kuwapatia viwanja mbadala, wananchi hao kushindikana, shauri hilo limepangwa kuendelea kusikilizwa tarehe 5 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua shauri hilo na kauli yetu ni kwamba tusubiri mwongozo au maamuzi ya mahakama ili tujue hatua zinazofuatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; baadhi ya wananchi waliovunjiwa nyumba

hizi tayari walikuwa na hati ambazo zilikuwa zimetolewa na Serikali. Sasa je, Serikali haioni imefanya maonezi makubwa kwa kuwavunja wananchi ambao tayari walikuwa na hati zilitolewa na Serikali yenyewe? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili nataka kujua sasa ni lini Serikali itatoa viwanja mbadala kwa wananchi hao ili kutokuwaumiza kama walivyofanya sasa? Nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la hati miliki pia kuhusiana na suala la pili la viwanja mbadala kwa kuwa jambo au shauri hili liko mahakamani, ningeomba tuwe na subira na tutakapopata mwongozo wa mahakama tutakuja kueleza hatua zinazofuatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Nani anazungumza sijamwona, Mheshimiwa Ally Makoa, sawa.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu, lakini majibu kutoka upande wa Serikali. Nilet matangazo niliyonayo hapa mbele halafu tuendelee na ratiba.

Tunao wageni ambao wametembelea Bungeni asubuhi hii. Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika.

Wapo wageni wanne wa Bunge kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) wakiongozwa na Askofu Mameo Ole Paulo, wote wasimame kwa pomoja, karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Tunao wageni wawili wa Bunge wa Bunge kutoka Fresh Spring Fellowship Church wakiongozwa na Mussa Richard Mwacha ambaye ni Mchungaji Kiongozi, karibuni sana. (Makofi)

Tunao wageni wawili wa Bunge kutoka Ubalozi wa Marekani nchini ambao ni Ndugu Kristin Mencer ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Siasa

Ubalozi wa Marekani Nchini, asimame kwa pamoja na mwenzake, karibuni sana. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni mwingine wa Bunge ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Bara, Ndugu Doroth Semu, karibu sana. (Makofii)

Tunaye mgeni wa Bunge mwingine ambaye ni Katibu Mkuu wa CUF Taifa, Ndugu Hamad Masoud Hamad, karibu sana. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao tungependa kuwatambua kwa pamoja, wageni wetu wote wa Waheshimiwa Wabunge, wote msimame kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu. Nadhani mmepata nafasi ya kujifunza mawili matatu kutoka kwenye Bunge lenu, karibuni sana, mnaweza kuketi. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wageni kutoka Taasisi ya *Tanzania in Protecting Society* kutoka Jijini Dodoma - karibuni sana. Tunao wageni 13 wa Women Voice and Connection kutoka Mkoani Morogoro, karibuni sana. Wapo Wanafunzi 22 na walimu watatu kutoka Chuo cha Ufundis Nangwa kilichopo Mkoani Manyara, karibuni sana. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulionao Bungeni siku ya leo, lakini ninayo matangazo mawili, moja linatoka kwa Katibu wa Bunge kwamba, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeweuka dawati katika viwanja vya Bunge nyuma ya Ukumbi wa Msekwa ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kufanya uhakiki wa taarifa za anuani za makazi zilizotolewa mwezi Februari hadi mwezi Mei, 2022.

Waheshimiwa Wabunge, kuna Wabunge naona wanahama viti, kuna Wabunge wanasimama, kuna Wabunge wanatembea. Waheshimiwa Wabunge mpo mnaotembea, mpo mnaozungumza na mko mnaohama viti. Nikiwa nimesimama hapa mbele mnasikiliza kwa sababu, huenda ninachokisema ni jambo lako wewe, ndiyo lengo hasa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhakiki taarifa zenu za anuani za makazi. Fursa hii Waheshimiwa Wabunge tuitumie vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania. Mnatangaziwa Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kuwa, leo tarehe 22 Septemba, 2022 mara baada ya kuahirisha Kikao

cha Bunge, mchana, kutakuwa na semina kwa Wabunge wanawake wote. Semina hiyo, imeandaliwa na Wakala wa Nishati Vijiji (REA) na itafanyika katika Ukumbi wa Kambarage uliopo jengo la Hazina, karibu na ukumbi wa JK Convention Centre. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuhuduria semina hii muhimu, ili muweze kuwatendea haki watu ambao mnawawakilisha hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo ya wageni tutaendelea na ratiba iliyombele yetu. Hapa alisimama Mheshimiwa Ally Makoa akiomba Muongozo kwa hivyo, kabla hatujaendelea nitamsikiliza ni jambo gani ambalo limefanyika mapema leo hapa, ambalo anataka kujua kama linaruhusiwa au haliruhusiwi, Mheshimiwa Ally Makoa.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, wakati swalii langu namba 118 likijibiwa na Mheshimiwa Waziri, nilitaka kujua kama Serikali ina mpango wa kubadilisha mwelekeo wa barabara ambayo imetajwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Serikali wa miaka Mitano pia imeelekezwa na Ilani Chama cha Mapinduzi. Kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kabisa wamekwenda tofauti na Ilani inavyosema na Mpango wa Serikali, wamechepusha barabara kule ambako wananchi hawakutegemea kwamba itaenda kule.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua mwongozo wako kwamba, kama jambo hili la Serikali kuamua kufanya mambo tofauti na mwongozo wa Serikali, mpango wa Serikali wa miaka Mitano na Ilani ya CCM, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Ally Makoa akieleza kuhusu majibu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye swalii ambalo yeye alikuwa ameliuliza, swalii la msingi namba 118, halafu anasema aliuliza maswali mengine ya nyongeza ambayo yalikuwa yanataka kujua kama Serikali imebadili mwelekeo wa ujenzi wa barabara. Anasema kwa majibu yaliyotolewa yameashiria kwamba, mabadiliko yamefanyika kwenye mwelekeo wa barabara hii. Anataka kujua sasa Kikanuni kama jambo hili je, linaruhusiwa au haliruhusiwi na ameeleza kwa kirefu kwamba, sehemu ambayo anataka kujua kama inaruhusiwa au hairuhusiwi, kwanza ni kubadili mpango wa miaka mitano, kwamba, katika ule mpango wa miaka mitano barabara muelekeo ni mwingine na sasa majibu yanaashiria kwamba uelekeo ni mwingine.

Sasa ukiacha mpango wa Serikali, pia ameeleza kwamba, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio inaiongoza Serikali na yenyewe ina

mwelekeo kama ule wa mpango wa miaka Mitano pia, anaeleza kwamba inaenda tofauti na mategemeo ya wananchi. Mwisho kabisa ameuliza kama jambo hili linaruhusiwa kufanywa na Serikali?

Waheshimiwa Wabunge, llani ni ya Chama cha Mapinduzi kwa hyo, maswali mengine tunaweza kuulizana huko kwenye Chama, lakini yale ambayo ameyauliza Mheshimiwa Mbunge hapa ametaka kujua kama Serikali inao uwezo wa kubadili mwelekeo wa barabara?

Waheshimiwa Wabunge, jibu ni kwamba, ndiyo, Serikali inao uwezo wa kubadili muelekeo wa barabara. Kwa hiyo, kama kuna jambo la ziada la hapo sasa ni la Mheshimiwa Mbunge na watu wako kule mtazame namna ambavyo Serikali ina sababu gani za kubadili muelekeo, kwa sababu sisi hatufanyi kila kitu na ndiyo maana Serikali ikileta hapa inafanya marekebisho hapa na pale na ndiyo maana mipango yetu tunaiweka kwa ajili ya kutuongoza lakini siyo kwamba ni msahafu kwamba, lazima iwe hivyo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Serikali huwa inaangalia mambo mengi na ndiyo maana inaweza ikasema inajenga barabara hii kwa kiwango cha lami, halafu haikujenga lami ikatumia zege kwa sababu, inaona mazingira yale pengine hata lami haitafaa. Sasa tukiweka mazingira ambayo Serikali itakuwa haiwezi kubadili hata nukta inaweza ikawa mtihani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa maana ya Mwongozo kwa namna majibu yalivyotoka, ndiyo Serikali inaruhusiwa kufanya hayo mabadiliko ya mwelekeo, sababu itakuwa nazo sasa kama zingeulizwa sababu nafikiri Naibu Waziri angeeleza hapa sababu kwa nini wamebadili mwelekeo, lakini kwa maana ya Mwongozo wa Kiti kama inaruhusiwa au hairuhusiwi, ndiyo, inaruhusiwa Serikali kubadili mwelekeo wa barabara. Ahsante sana. (Kicheko/Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, ili tuendelee na ratiba hiyo, nitamuita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene ili aweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni tuweze kutoa fursa kwa ajili ya jambo linalofuata baada ya hapa. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:**  
**SPEAKER:** Thank you so much. Those were the questions from the Members of Parliament, and so, now I give you 30 seconds to wind up and then you can take your leave.

**MR. MOHAMED M. NGULANGWA:** Honorable Speaker, the late President of Tanzania, Dr. Magufuli used to say that: "maendeleo hayana chama." I stand before you to request for the votes because it is competence that is required in the East African Community. Kindly vote for me.

**SPEAKER:** Thank you so much. You may now take your leave.  
(Applause)

**SPIKA:** Katibu, anayefuata.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, anayefuata ni Ndugu Thomas Malima.

**SPEAKER:** Mr. Thomas Malima, before you are the Members of Parliament of Tanzania and they would like to hear from you why they should elect you to be the country's representative in the East African Legislative Assembly. You have three minutes to express yourself and convince the House. Please, you have the floor.

**MR. THOMAS D. C. MALIMA:** Honorable Speaker, Prime Minister and other Honorable Members of this Parliament of Tanzania, thank you.

Honorable Speaker, first of all, I have to introduce myself to you. My name is Thomas D.C. Malima. I am a graduate of a Bachelor of Arts with Education from the University of Dar es Salaam. And through that education, I am also a Head of School in Kigoma.

Honorable Speaker, I am here to vie for the post of representing our Nation in the East African Legislative Assembly due to the fact that first of all, I am a Tanzanian, I have the right to contest for this position; I am also capable to contest for it and to represent the Nation at the Assembly.

Honorable Speaker, I know the function of this assembly is to discuss various agenda and motions which are tabled in the Legislative Assembly. Also, the Assembly is responsible to discuss and approve the budgets of all organs of the East African Community. And so, therefore, as a member of the East African Legislative Assembly, if you will elect me to be a member, first of all I will coordinate and communicate with other elected members from Tanzania to take the National interest to the Legislative Assembly. (Applause)

Honorable Speaker, here, we need a person who is loyal to the Nation, a person who is cooperative to the Government, a person who knows the

resources of the Nation and how to protect them. I am the one whom is able to cooperate with other members who will be elected to be a member of the Legislative Assembly for the interest of the Nation in order to make it grow.

Honorable Speaker, also, as a member of the Legislative Assembly, I will make sure that I will take directives from the Ministry responsible for the East African Community affairs in order to make sure that when we are discussing issues in parliament, we will discuss according to the National privileges and priorities.

**SPEAKER:** Thank you so much. There is only one Member interested in asking you a question. Honorable Ally Mchungahela.

**HON. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Thank you Honorable Speaker. This region has been one of the dumping places of the market, what are the strategies you have to alleviate the problem? Thank you.

**MR. THOMAS D. C. MALIMA:** Honorable Speaker, there was noise, I did not understand the question.

**SPEAKER:** Members of Parliament, he is saying he didn't hear you. Honorable Ally Mchungahela, can you repeat yourself please.

**HON. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Yah. What I asked is; this region is among the dumping places of the foreign market, what is your strategy to alleviate the problem of dumping in this region of the East African Community?

**SPEAKER:** Honorable Members, I will rule that out as a question to the candidate. And I see no other Member of Parliament rising up to ask a question. So I give you 30 seconds to wind up and then you may take your leave. Thank you.

**MR. THOMAS D. C. MALIMA:** Okay. Thank you, Honorable Speaker. As I have introduced myself to you, I am vying for this post because I know there are some issues which we are going to discuss, not for my own views but the National views to the community. Even the issue of markets, together with other elected members, with the Government of Tanzania, we will come up with a strategy to make sure that, it will be our strategy in the East African Legislative Assembly. Through that strategy, we will make sure that our Nation benefits from the community and also the East African Community benefits, and that we will prohibit the dumping of commodities from non-East African.

Thank you. (Applause)

**SPEAKER:** Thank you so much Mr. Malima, you may now take your leave. (Applause)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu ndio alikuwa mgombea wa mwisho kuja kujieleza mbele yetu. Sasa tunaelekea kwenye zoezi la kupiga kura. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge wote walioko nje waingie ndani ili tuhesabiane. Tukishamaliza hesabu, Mbunge aliyeko nje, kwa sababu tunataka kutenda haki, hataruhusiwa kuingia tukishamaliza hesabu ili tuisumbuke kwenye kuhesabu kura. Wabunge wote walioko nje waingie ndani, zoezi la kuwahesabu linaanza mara moja.

Katibu, tunahitaji kujua ni wangapi. Waheshimiwa Wabunge, tuwe watulivu kidogo wakati tunaendelea kuwasubiri wenzetu walio nje, nawaona wanaendelea kuingia, ili tupate hesabu yetu kamili kabla hatujaanza kupiga kura.

Haya, wakati hesabu inaendelea kupigwa hapa, Katibu na timu yake waendelee kuijandaa kwa sababu zoezi la kupiga kura linapoanza karatasi zitagawiwa. Kwa hiyo, maandalizi yaendelee wakati nasubiri hesabu hapa mbele.

Haya. Waheshimiwa Wabunge, sasa milango hiyo haitafunguliwa, nimeshaletewa idadi ya Wabunge waliopo. Kwa hiyo, wasaidizi, milango ya kutoka na kuingia hapa ndani iko mitatu, mijipange vizuri ili kama mtu yuko nje, niletewe kwanza taarifa hapa ndiyo aingie humu ndani ili tusije tukapata changamoto kwenye kuhesabu kura. Wasaidizi mijipange kabisa milangoni, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, idadi ya Wabunge tulipo tayari kwa ajili ya kupiga kura ni 300. Wabunge tumehesabiwa na tuko 300. Kwa hiyo zoezi la kupiga kura litaanza sasa. Katibu na timu yako tunahitaji sasa makaratasi yaanze kugawiwa. Tuko Wabunge 300, kama kuna Mbunge anaongezeka, asiingie kabla sijapewa taarifa hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge wakati wanawaletea hizo karatasi mtapewa karatasi za kupigia kura nne kulingana na makundi yale manne na kila karatasi imeandikwa upige kura ngapi. Kundi la kwanza, unapiga kura tatu kati ya majina sita na mtayaona hapo. Kundi la pili, mnapiga kura mbili kati ya hao watano walioko kwenye hiyo karatasi ya kura na kundi la tatu, mtaona majina yako matatu mnatakiwa kupiga kura moja na kwenye karatasi pia imeandikwa. Kundi la nne mnatakiwa kupiga kura tatu kati ya wagombea sita waliopo.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kwenye sehemu ya kupiga kura tatu ukipiga nne kura imeharibika. Nadhani hili limeeleweka na kwenye kura moja ukipiga mbili imeharibika. Kwenye kura mbili ukipiga tatu imeharibika hivyo hivyo na nyingine zote.

Wasaidizi sasa mtawanyike tayari kwa kugawa kura. Sasa ngoja tuelowane, nyinyi mlioshika karatasi mmeshika za kundi moja moja? Mmeshika karatasi za kundi moja moja au makundi yote? Wewe umeshika makundi mangapi.

**MSAIDIZI WA BUNGE:** Kundi moja.

**SPIKA:** Kundi moja?

**MSAIDIZI WA BUNGE:** Ndiyo, kundi A.

**SPIKA:** Kundi 'A' na yule kule nyuma?

**MSAIDIZI WA BUNGE:** Hakusikika.

**SPIKA:** Sasa kama hivyo ndivyo Katibu ngoja, njoo. Kama ndivyo kama mnagawa moja moja nendeni kwa pamoja ili mnampa huyu nne, mpaka tutakaposema nani hajapata tutajua hajapata karatasi ipi vinginevyo tutachanganya mambo.

Hebu njoo huku usichukue hiyo karatasi, iache tu haina neno, wewe njoo huku mbele. Wale walioshika kundi A ni wapi?

**MSAIDIZI WA BUNGE:** (*Hapa hakusikika*).

**SPIKA:** Haya kundi la kwanza, jamani muwe mnanisikiliza huku. Wewe nawe umeshika ya kwanza?

**MSAIDIZI WA BUNGE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Huyu?

**MSAIDIZI WA BUNGE:** Kundi C.

**SPIKA:** Wewe sogea nyuma kidogo C.

Wewe je?

**MSAIDIZI WA BUNGE:** Kundi A.

**SPIKA:** Kundi A sogea.

Sasa mfuatane kwa mtindo huo, ngoja, anzieni hapa kwa Mheshimiwa Sanga, mpeni, hakikisheni anapata karatasi nne za makundi yote, mnakwenda namna hiyo. Kwa sababu mkitawanyika hatutajua mnakwenda kugawa kura namna gani, sijui nimeeleweka? Yaani anavyopita A anapita

na B anapita na mwingine, kwa hiyo, mwingine aanzie pale kwa Waziri Mkuu A, B, C, D pale, kwa hiyo mnakwenda kwa makundi namna hiyo.

Haya, Mheshimiwa Sanga una karatasi ngapi? Nne? Profesa hapa wameongozana Maprofesa, Daktari, nne?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya sawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ufanuzi. Ufanuzi wa jinsi ya kupiga kura.

**SPIKA:** Ufanuzi karibu.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, ulikuwa unatangaza ufanuzi wa kupiga kura nilitaka kufahamu katika *ballot paper* imeonesha kwamba kuna sehemu unapiga watu watatu, umesema mkipiga watu wanne kura imeharibika. Je, katika watatu nikiamua kumpigia mmoja?

**SPIKA:** Sawa. Sasa masharti tuliyoweka kwenye hizi karatasi za kura na masharti aliyokuwa ameyasoma Katibu mapema, karatasi inaelekeza hivi; kwa mfano Kundi 'A' inasema piga kura tatu tu kwa kundi hili. Weka alama ya Vema. Sasa kwa sababu nimesema piga kura tatu, haijasema piga angalau, piga kura tatu, usianze hapa namtaka mmoja tu. Kwa sababu zinatakiwa tatu ndio hesabu zetu ziende vizuri, wewe nani ambaye haujamsikia hapa mpaka upige kura pungufu, jamani! Si mmesikia wagombea hapa jamani, yaani wewe ukose watatu kati ya hawa kweli, haiwezekani!

Haya Waheshimiwa Wabunge zoezi la kugawa makaratasi limeshaanza na sasa naambiwa wako Wabunge nje wanasubiri kuingia sasa kama nilivyosema, zoezi letu ni la wazi, nataka kujua wako wangapi upande huu wako wangapi? Ngoja, ngoja Mheshimiwa Mariam Kisangi nakuona unaingia ulikuwa umeshahesabiwa au hapana? Kwa sababu, wewe msaidizi hapo mlangoni ndio unataka kunichanganya, lazima nipewe taarifa au ametoka upande huu anahamia huku?

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, nimetoka huku.

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa, shukrani. Haya huku Mheshimiwa Mwakagenda anaingia na natakiwa nipate taarifa kama alishahesabiwa au hapana? Mheshimiwa Mwakagenda wakati tunahesabu ulikuwepo ama hukuwepo?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Sikuwepo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ile 300 inakuwa 301. Tumeshasikilizana Mbunge mmoja ameongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Kamwelwe naona umesimama. Sema na kisemeo.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Spika, wakati wajumbe wanahesabiwa nilikuwa nje.

**SPIKA:** Mheshimiwa umepita mlango upi? Maana isije kuwa walikuhesabu halafu hapa nikaongeza idadi isije ikaleta changamoto. Umepita upande upi?

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Spika, upande huu.

**SPIKA:** Upande huu.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Haya kwa hiyo 302.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge asiingie hata nyinyi wasaidizi huko milangoni asiingie mtu kabla sijaambiya.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, mlango mkubwa kuna Mheshimiwa Zaytun Swai alikuwa hajahesabiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, tunakuwa na 303. Hapo wanakuwa wameongezeka Wabunge watatu zaidi, kwa hiyo 303 jumla.

Waheshimiwa Wabunge narejea tena, la sivyo mtakuwa hampigi kura na ni haki yenu ya msingi. Kama hukuwepo wakati wa kuhesabiwa wasaidizi wa milangoni mnaniangusha, asiingie mtu Bungeni kabla sijapewa taarifa. Haya Wabunge ambao walikuwa hawajahesabiwa, naona Mheshimiwa Rita Kabati umesimama umepita mlango upi? Msaidizi hapo mlangoni unahitaji msaidizi mwenzio aongezeka maana unaingiza watu wengi sana na huniambi.

Haya namwona Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Rita Kabati, Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mheshimiwa Mary Masanja hao ni Wabunge wanne wameongezeka. Kwa hiyo, tunakuwa na 307.

Msaидизи улиyепо upande huu Mbunge аsiингie kabla sijapewa taarifa, nadhani hilo limeeleweka?

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama nimehesabiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sawa. Sasa hili zoezi naona linakuwa gumu, kama mtu anasema hajui ama anajua. Hakuna neno, tusiwe na wasiwasi hapa nina idadi ya 307, lakini nimeshaagiza wasaidizi wahesabu tena sasa hivi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge karatasi mnazopokea kupiga kura hakujatangazwa bado, naona kuna watu mmeanza kuweka tiki huko. (Kicheko)

Subirini wote tupate karatasi kwa sababu kama zitakuwa karatasi zimepelea zoezi litatusumbua kidogo kwa hiyo, subirini kidogo.

Wagawa karatasi ongezeni bidii/ongezeni spidi wagawa karatasi. Upande wangu wa kulia kuna mtu hajapata karatasi?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ndio hapa hakuna karatasi, karibu zote hazipo hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere maana yake umeingia baadaye, jirani yako mbona anazo?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, hapana ni hizo hizo tumepewa mbili tu, hakuna karatasi nyingine ya tatu.

**SPIKA:** Umepewa ngapi?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, mbili tu na wasaidizi wameshaondoka wamekwenda upande wa pili.

**SPIKA:** Haya ngoja nisaидие Mheshimiwa Getere nisomee za kwako ni kundi gani na kundi gani?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Kundi 'B' na Kundi 'A'.

**SPIKA:** Bado 'C' na 'D', jamani makaratasi 'C' na 'D' upande huu bado hayajafika.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hata huku bado.

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hata kuhu.

**SPIKA:** Mbili au tatu?

**MHE. FULANI:** Hata huku bado tumepata mbili tu.

**SPIKA:** Haya ngoja twende vizuri nyinyi mnaogawa makaratasi nisikilizeni mtu ambaye ana Kundi 'C' na 'D' hebu anyooshe mkono 'C' na 'D' sio Wabunge wanaogawa karatasi 'C' na 'D' nani wanazo? Wewe mwenye 'C' hapo katikati wewe unayeongea na Mheshimiwa Neema Mgaya una Kundi gani? Njoo umalizie kwanza huku.

Mwenye Kundi 'D' nyinyi wasaidizi wa Katibu mwenye Kundi 'D' mmoja arejee huku, malizeni kwanza upande huu, maliza hapa, halafu fuata panapofuata. Rudi hapa anzia hapa, haya kule nyuma nani hana nne?

Haya upande wangu wa kulia hapa kuna mtu hana karatasi na ni ya kundi gani?

**MBUNGE FULANI:** Sina ya Kundi C.

**SPIKA:** Sawa, kundi 'C' huna, huyo wa nyuma yako ana nini? Haya 'C' yule pale akupe. Kuna mtu hana hapo mbele. Subirini zinakuja, zinakuja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, Kundi 'D' hakuna.

**SPIKA:** Haya upande wangu wa kulia hapa kwa Mawaziri na wajumbe wengine kule nyuma kuna mtu hana karatasi yoyote hapa? Wote mnazo nne? Mheshimiwa Massay wote mnazo nne sasa? Bado ipi?

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina ya Kundi D.

**SPIKA:** Haya, Kundi 'D' mpelekee karatasi Mheshimiwa Janeth Masaburi.

Haya Waheshimiwa Wabunge mlion nyuma ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kila mtu ana karatasi nne?

Jamani mnaojibu hamko nyuma ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nyinyi wote mnazo hapo?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, hakuna ya Kundi B.

**22 SEPTEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati hauna karatasi gani?

**MHE. DKT. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ya Kundi A.

**SPIKA:** Haya ‘A’ huku mbele mpelekeeni karatasi Mheshimiwa Rita Kabati. Yule anayegawa ‘A’ ampelekee karatasi Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, ‘B’ hatuna hapa.

**SPIKA:** Nani anayezungumza? Haya Mheshimiwa Janeth Masaburi umeshapata?

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, bado Kundi ‘A’? Jamani Kundi ‘A’ mtafutieni karatasi Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Kundi ‘B’

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, hatujapata ‘A’, ‘B’ wala ‘C’.

**SPIKA:** Sijui ni nani anazungumza? Nani anayezungumza?

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete huna karatasi gani naona umenyoosha?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** (Hapa hakusikika).

**SPIKA:** Okay, upande wangu hauna karatasi gani Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ‘B’.

**SPIKA:** ‘B’ haya.

Modesta mtafutie karatasi ‘B’ Mheshimiwa Naibu Waziri. Haya upande wangu wa kulia Mheshimiwa Mkuchika una karatasi nne?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Upande wangu wa kulia kuna mwenye karatasi pungufu ya nne? Hakuna.

Mheshimiwa Neema Mgaya huna karatasi namba ngapi?

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, kundi D.

**SPIKA:** Namba ‘D’ mwenye karatasi ‘D’ awape Mheshimiwa Neema, Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Hussein.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, sijapewa ya Kundi B.

**SPIKA:** Sijui uko upande gani nani ambaye hajapewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hajapewa ya Kundi B. Halafu Waheshimiwa Wabunge niwaombe tuwe na utulivu kidogo, watu niliowapa kazi ya kuhesabu inabidi warudie tena kwa sababu kuna Wabunge wanahama.

Kwa hiyo, wanahesabiwa huku wameshahama kiti na kwa hivyo tena zoezi linakuwa gumu kweli. Kwa hiyo tuwe na utulivu wamalize kazi ya kuhesabu. Ndugu Kizingiti na wengine wote peaneni raw moja moja, sawa? Anzieni hapa ambapo watu wana utulivu halafu muendelee. Mheshimiwa Mbunge ukishapewa karatasi ukitoka sasa Kiti tena kitahesabiwa kitupu mbona shughuli. Mheshimiwa Rose ingia kwa sababu wanaanza kuhesabu upya tena.

Mheshimiwa Mbunge upande wangu wa kulia ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ambao mmekaa upande wa Mheshimiwa Najma ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono. Mheshimiwa Rose hiyo ndiyo seat yako au huwa unakaa huku? Kama unakaa huku njoo kwenye seat yako tafadhalii.

Waheshimiwa Wabunge, waliokaa nyuma ya Mheshimiwa Kingu ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono. Waheshimiwa Wabunge wanaokaa eneo ambalo yuko Mheshimiwa Katani huku mbele ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kambi ya walio wachache ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono, haya malizieni hapa mbele hawa wawili hawana karatasi Nne. Mheshimiwa Mbunge yejote ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono, haya hapo mbele malizia hao wawili, huna karatasi

gani kule nyuma sikuoni vizuri, Mheshimiwa kule nyuma washa kisemeo. Haya Mbunge ambaye hana karatasi Nne anyooshe mkono. Wagawa karatasi pale nyuma kamsaidieni Mheshimiwa Rose Busiga pale hana karatasi hata moja, mpelekeeni karatasi za kura.

Waheshimiwa Wabunge, kuna yeote ambaye hana karatasi, hakuna. Sasa niwaombe ili tuweze kwenda na zoezi letu kwa haraka hizo karatasi 4 hazitakusanya kwenye box moja, karatasi 4 usitumbukize kwenye box moja. Watu watapita na box moja moja kwa aina ya kundi uliopiga kura. Sasa tunaanzia upande wangu wa kulia ambako ndio tulianza kugawa karatasi, kwa hiyo kura zipigwe sasa na tutaanza kukusanya kundi A. Msaidizi mwenye box la kundi A abebe sasa, kusanya kundi A pekee.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tuwe tunasikilizana hilo nalo ni kundi gani? Sawa. Hawa wanaopita sasa wanakusanya kundi A pekee usikusanye zaidi ya kundi A. Haya piteni. Sasa pia mwende vizuri maana atabaki huku tena mtu ana A malizeni hapa, mnaelekea kwingine. Sasa huku kwa kuwa mko wengi; kundi A pekee tafadhali. Tunakusanya kundi moja A pekee usipoteze kura yako.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya uhakiki wa Bunge kwa ujumla wetu tuko 322. Mheshimiwa Sanga umenyoosha karatasi hiyo ni B au A? aah tayari ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ambaye bado ana karatasi A mkononi anyooshe juu. Haya kundi A mnaokusanya karatasi ongezeni mwendo. Jamani wakusanya karatasi hebu changamkeni mko wengi sana. Haya kundi A kama mmemaliza kukusanya rejeeni huku mbele nani ana karatasi la kundi A bado? Kundi A rejeeni huku mbele na ma-box. Kule nyuma Modesta kuna mtu hajapiga kura au shida iko wapi?

Waheshimiwa Wabunge, tunawatangazia ili muandae karatasi zenu mapema la sivyo hili zoezi litakuwa gumu sana. Humu ndani si tunajua jamani kusoma na kuandika au? Kuna mtu haioni A? haya tafadhali kusanyeni hizo kura zote kwenye box moja kundi A. Haya funika hizo kura tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, kundi B sasa. Kundi B ninyi mko wengi anzia upande huu wawili, kundi B, Modesta huku, wawili huku, haya. Anzia hapa ndiyo maana mnachanganya mambo au zimejikusanya pemberi. Haya tunaanza kukusanya kundi B sasa.

Waheshimiwa Wabunge, ushauri kwa sababu kura ni siri na umeifunga mpe mtu wa pemberi kuliko kumfanya mtumishi azunguke kwenye viti. Kura ni siri na umeifunga mpe mtu wa pemberi ili wapite kwenye hayo maeneo ya kupita. Kunja kura yako mpe mtu wa pemberi hatoifungua. Haya Wabunge ambao bado hawajakusanya kundi B, haya zipelekeni pemberi

upande anaopita mhudumu ndio peleka upande huo. Mheshimiwa Kitila ndio uko pemberi tukusanyie kura naona majirani zako bado wanapeperusha hapo. Aah! msichanganye mambo C hatujaanza. Wenye karatasi B wanyooshe juu, haya B rejeeni huku mbele kama mmemaliza kukusanya faster. B rejeeni huku mbele na ma-box.

Waheshimiwa Wabunge, andaeni kundi C na pelekeni pemberi. Andaeni kura C na peleka kwa Mbunge aliyeko pemberi. Haya tunaenda vilevile kundi C sasa. Anzia huku wengine wawili waanzie huku. Nenda kwenye zile za katikati pale.

Waheshimiwa Wabunge, kura zikishakusanya hapa mbele tukisha-seal hatuwezi tena kuongeza kura hata kama ukisema umeipiga umesahau kukusanya. Kwa sababu sasa itaonekana tumegawa karatasi zaidi ya watu walioko humu ndani. Kwa hiyo, tunapotangaza kundi kusanya na kundi husika. sasa hivi tunakusanya kundi C. Haya wale ambao wameshamaliza kukusanya hizo waanze kuijandaa kukusanya kundi D. Haya kundi C rejeeni mbele haraka wekeni kwenye box ambalo limeandikwa kundi C.

Waheshimiwa Wabunge, anzeni kukusanya kundi D peleka kwa Mbunge aliyeko pemberi. Kundi D zinaanza kukusanya sasa. Haya mwenye karatasi D bado mkononi anyooshe mkono, mwenye karatasi D anyooshe mkono, haya zinakusanya hapo. Mwenye karatasi D ainyooshe juu ili ikusanywe. Haya D mlionenda kukusanya rudini huku mbele muweke kwenye box lililoandikwa.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshakusanya kura zote za makundi yote manne na zoezi sasa linalofuata ni la kuhesabu hizi kura na Kanuni zinanipa mimi mamlaka ya kuchagua watu ambao nataka wakanisaidie kusimamia hili zoezi la kuhesabu kura pamoja na wasaidizi kutoka Ofisi ya Katibu. Kwa hivyo, nimewateua Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Grace Tendega. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wawili hawa wataenda kutazama hilo zoezi la kuhesabu kura na wataongozana na hawa wengine ambao wanaenda kuhesabu, Katibu kwa namna mlivyojipanga sasa. Wale mlioteuliwa kwenda kuhesabu kura muongozane. Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, naona kuna Wabunge wanajiliza tatizo, ndio maana huwa nasema nikisimama hapa muwe mnanisikiliza kwa sababu kuna maswali mnauliza ambayo yameshasomwa utaratibu hapa. Wagombea wapo 20 mnataka kila mgombea akawe na wakala, Kanuni yetu ya 11 inaeleza utaratibu na mmesomewa humu humu ndani na ndio maana wameteuliwa hao wawili kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi, msiwe na wasiwasi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kura zimeenda kuhesabiwa kwa kutumia Kanuni ya 5 ambayo inanipa mamlaka ya kutazama uendeshaji bora wa Bunge na mambo ninayoona. Sasa hapa tuna ratiba mbele yetu na wagombea kama mlivyoona wako 20 kwa hiyo kila mtu lazima ahesabiwe kura zake zoezi ambalo litatuchukua muda kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa kutazama ratiba yetu tuna ratiba manake baada ya uchaguzi bado kuna mambo mengine yanapaswa kuendelea. Sasa kwa kutumia mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 5 pamoja na kwamba ninayo yote ninaweza kufanya maamuzi lakini nimeamua kufanya maamuzi leo ya kidemokrasia. Kuna namna mbili aidha tuendelee na ratiba iliyoko hapa tukisubiri matokeo au turudi Saa Kumi na Moja tupewe matokeo na tuendelee na ratiba. Sasa demokrasia tuendelee na ratiba ama turudi Saa Kumi na Moja.

**MBUNGE FULANI:** Tuendelee na ratiba.

**SPIKA:** Tuendelee na ratiba.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 (The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ilikuwa imeshawekwa Mezani asubuhi. Hivyo, nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mcembba, aje atoe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 (The Written Laws (Financial Provisions) (Amendment) Act, 2022) pamoja na Marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri mbalimbali iloi kuboresha. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru pia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho kwenye sheria zinazosimamia kodi na mrabaha kwa kubadili viwango vya kodi pamoja na mrabaha na kuweka taratibu za utoaji vivutio kwa wawekezaji, ili kuhamasisha uzalishaji kwa viwanda vya ndani vya nchi vya mbolea pamoja na magunia ya mkonge pamoja na kuondoa changamoto zilizopo hivi sasa katika utekelezaji wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura Na. 38.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni sheria zifuatazo:-

- (1) Ushuru wa Bidhaa, Sura Na. 147;
- (2) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332;
- (3) Sheria ya Madini, Sura Na. 123;
- (4) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Na. 220; na
- (5) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Na. 148.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Muswada; Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Sita, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekeblishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada yenyewe Ibara ya 3 hadi ya 5 inapendekeza kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Na. 147 ambapo Kifungu cha 128 kinapendekezwa kurekeblishwa ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, baada ya kupata idhini ya Baraza la Mawaziri, kusamehe ushuru kwenye bidhaa zitakazotumika katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji mahiri na mahiri maalum, inayoidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (NISC).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, iwapo itabainika kwamba, msamaha uliotolewa kwa mwekezaji umetumika tofauti na malengo yaliyokusudiwa, msamaha huo husika utafutwa na mwekezaji atalazimika kulipa kodi iliyosamehewa. Marekebisho hayo yanayopendekezwa yanalenga kuwianisha masharti ya sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania ili kuboresha utekelezaji wa vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile sehemu hii inapendekeza kurekebisha Jedwali Na.4 la sheria hii kwa kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo unaotokana na zao la zabibu, unaoingizwa kutoka nje ya nchi kutoka Sh.2,466.45 kwa lita hadi Sh.5,600 kwa lita. Lengo la marekebisho haya

yanayopendekezwa ni kuwezesha mvinyo unaozalishwa na zabibu zinazolimwa hapa nchini kuweza kushindana kwenye soko la ndani na mvinyo unaotoka nje ya nchi. Hii itasaidia kuhakikisha upatikanaji wa soko la zabibu zinazolimwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wakulima wa zabibu nchini, hususan wakulima wa Mkoa wa Dodoma wanashindwa kupata soko la uhakika kwa mazao kwa kuwa viwanda vya ndani vinavyozalisha mvinyo ambavyo ndio wanunuzi wakuu wa zabibu yao vinakosa soko la kuza mvinyo wanaozalisha kutokana na ushindani wa mvinyo unaotoka nje ambaa unauzwa kwa bei rahisi, ikilinganishwa na mvinyo unaozalishwa hapa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 332, ambapo Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kujumuisha uwekezaji mahiri ulioihinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji katika wigo wa maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya mapato. Lengo la marekebiso haya yanayopendekezwa ni kuwianisha masharti ya sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania ili kuboresha utekelezaji wa vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji. Hata hivyo, marekebiso yamefanyika katika Muswada ili kubainisha kwamba, Serikali inafuta msamaha husika pindi itakapojiridhisha kwamba, msamaha husika haukutumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebiso katika Kifungu cha 87(1) cha Sheria ya Madini, Sura Namba 123, ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwa malighafi za mbolea zinazochimbwa hapa nchini ambazo ni Phosphate O na Limestone kutoka asimia tatu hadi asilimia moja. Lengo la marekebiso haya ni kutoa nafuu kwa gharama za malighafi za wazalishaji wa ndani wa bidhaa za mbolea. Serikali ina imani kwamba, unafuu huu unaotolewa kwa wazalishaji wa mbolea utaleta matokeo chanya kwenye upunguaji wa bei ya mbolea kwa wakulima na hivyo kupunguza mzigo kwa Serikali katika utoaji wa fedha za ruzuku kwenye mbolea.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada kama ilivyofanyiwa marekebiso, inapendekeza kufanya marekebiso katika Kifungu cha 8 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Mafuta, Sura Na. 220, ili kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe ushuru wa mafuta kwa miradi ya uwekezaji mahiri na mahiri maalum itakayoidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji. Lengo la marekebiso haya ni kuwianisha masharti ya sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania ili kuwezesha utekelezaji wa vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba, mafuta yanayopewa msamaha hayatumiki vibaya, hati za msamaha wa kodi zinazotolewa, pamoja na mambo mengine, zitabainisha muda wa kuanza na kumalizika kwa msamaha husika, kiwango cha mafuta kinachopewa msamaha pamoja na mradi unaonufaika na msamaha. Vilevile Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itaweka utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye miradi husika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wizara ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji, Kituo cha Uwekezaji Tanzania na wadau wengine wa Serikali ili kuhakikisha kwamba, mafuta husika yanatumika kama yalivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Namba 148, kama ifuatavyo:-

- (i) Kifungu cha 6 kinafanyiwa marekebiso ili kujumuisha uwekezaji mahiri ulioidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji katika wigo na maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Lengo la marekebiso haya ni kuwianisha masharti ya sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania kuhusu utoaji wa vivutio vya kodi kwa wawekezaji.
- (ii) Kuongeza Kifungu cha 55A kwa kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha sifuri kwa mbolea inayozalishwa ndani ya nchi ili kuleta unafuu kwa wakulima na watumiaji wa mbolea kwa kupunguza gharama za uzalishaji wa mbolea wa viwanda vinavyozalisha bidhaa hii hapa nchini. Hata hivyo, unafuu huu unatolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja tu ili kutoa nafasi kwa Serikali kufanya tathmini na kujiridhisha iwapo unafuu uliotolewa utawanufaisha wakulima, hususan, kwa kupungua kwa bei ya mbolea inayozalishwa hapa nchini.
- (iii) Inapendekezwa kurekebisha Jedwali la Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa magunia ya mkonge yanayotengenezwa nchini na yanayotambulika kwa HS Code 63059000. Lengo la marekebiso haya ni kuwezesha magunia ya mkonge yanayozalishwa na viwanda vya ndani kushindana na magunia yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Hatua hii itasaidia kuchochea kilimo cha mkonge hapa nchini, ajira kwa wananchi na kuongeza mapato ya Serikali.

Vilevile kufuatia majadiliano ya kina baina ya Serikali na Kamati ya Bajeti, inapendekezwa kupitia Jedwali la Marekebiso kuondoa pendekazo la kutoa msamaha kwa malighafi ya kutengeneza mitungi ya gesi inayotambulika kwa HS Code

72299000 na kutoa nafasi ya Serikali kufanya kazi zaidi mapendekozo husika ili kujiridhisha kwamba, malighafi husika haiwezi kutumika kwenye matumizi mengine na hivyo kupoteza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; kufuatia maelezo haya, naomba Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu na hatimaye wakubali kupitishwa kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana.

Kabla sijamwita Mwenyekiti wetu wa Kamati kuja kuwasilisha, tunaye mgeni ambaye aliingia baada ya matangazo ya wageni kuwa yameshafanyika ama yameshatangazwa. Huyu ni mgeni wa Bunge ambaye ni Mbunge Mstaafu na Kiongozi Mkuu wa ACT Wazalendo, Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe. (Makofi)

Sijui amekaa upande gani? Niliambiwa ameingia humu ndani, karibu sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, karibu sana. (Makofi)

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**

**YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha, Namba 13 wa Mwaka 2022 (*The Written Laws Financial Provisions Amendment Act. 2022*).

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Septemba, 2022 Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni mapendekozo ya Serikali kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha, Namba 13. Baada ya Waziri kuuwasilisha Muswada huo, Mheshimiwa Spika, uliagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuuchambua Muswada huo ili badae maoni yake yawasilishwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada; Kamati imefanya uchambuzi wa Muswada huu kwa kupitia kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujelimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekaze marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, tarehe 19 hadi 21 Septemba, 2022 Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara pamoja na watendaji wa Wizara. Aidha, Kamati pia ilikutana na wadau kwa ajili ya kupokea mapendekazo na maoni yao juu ya marekebisho yanayopendekezwa; wadau waliofika kwenye kamati ni Aliko Vintage.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya Muswada; Muswada huu una madhumuni makubwa matatu kama ifuatavyo:-

- (i) Kuchochea uzalishaji wa mbolea nchini ili ipatikane kwa bei naifuu;
- (ii) Kutoa vivutio maalum kwa miradi ya kimkakati na miradi mahiri ili kuchochea uwekezaji kwenye miradi mikubwa ili kuleta mapinduzi ya kiuchumi; na
- (iii) Kuchochea uzalishaji wa ndani, hasa wa bidhaa za magunia na mvinyo ili kuchochea kilimo cha mazao ya zabibu na katani.

Mheshimiwa Spika, kwa kutazama madhumuni haya ya Muswada huu nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuonesha nia ya dhati ya kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mikubwa itakayoleta mapinduzi ya uchumi. Kamati inaamini kwamba, kwa masharti yaliyoko kwenye Muswada huu Mheshimiwa Rais atakuwa ameonesha kwa vitendo namna bora ya kutanzua vikwazo vitakavyokwamisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati Kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha, Namba 13, wa Mwaka 2022; Muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria tano za kodi ambazo ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Madini, Sura ya 123; Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura ya 220; na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekazo yafuatayo:-

(1) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Serikali inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 128 ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, baada ya kupata idhini ya Baraza la Mawaziri, kusamehe ushuru kwenye bidhaa zitakazotumika katika utekelezaji wa miradi ya kiuwekezaji mahiri na ya kimkakati itakayoidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (NISC) pamoja na kupandisha ushuru wa bidhaa za mvinyo kutoka nje kutoka Sh.2,466.45 hadi Sh.5,600 kwa lita ili kulinda wakulima wa ndani wa zao la zabibu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa nchi za jirani zinatoza kati ya Sh.5,000 hadi 5,500 kwa lita ya mvinyo unaotoka nje. Hivyo, hatua hii inahuisha viwango vinavyotozwa katika Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki. Aidha, hatua hii inaleta usawa wa kiushindani kati ya wazalishaji wa zao la zabibu nchini dhidi ya mataifa mengine ambayo yameendelea sana katika uzalishaji wa zao hili. Hivyo, Kamati inakubaliana na pendekезо hili ambalo lina nia njema ya kusaidia na kuinua viwanda vya ndani na kuwa shindani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ubora wa mvinyo unaozalishwa ndani ya nchi pamoja na kuchochea kilimo cha aina mbalimbali za zabibu ili kuhakikisha kwamba, malighafi hii muhimu kwa utengenezaji wa mvinyo inapatikana ndani ya nchi. Aidha, Kamati iliishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti kwamba, endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo haijokusudiwa msamaha huo utaondolewa na mhusika atalazimika kulipa ushuru stahiki. Marekebisheso haya yanaonekana kupitia Jedwali la Marekebisheso ya Serikali.

(2) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 532; Kifungu cha 10 kinarekebisheswa ili kujumuisha uwekezaji mahiri ulioidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji katika wigo wa maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya mapato. Aidha, mapendekezo haya yanabainisha kwamba, misamaha ya kodi ya mapato itakayokuwa inatolewa kupitia mikataba ambayo Serikali inaingia ndio itatumika wakati wa kukokotoa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ina nia njema ya kutanzua mkwamo wa miradi ya kimkakati ya uwekezaji mahiri. Uzoefu unaonesha kuwa kuna baadhi ya wawekezaji mahiri wametumia mikataba yao vibaya na kuhakikisha kwamba, Serikali haipati mapato yake inayostahili. Aidha, Kamati iliishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti la kwamba, endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo haijokusudiwa, msamaha huo utaondolewa. Marekebisheso haya yanaonekana kupitia Jedwali la Marekebisheso la Serikali.

(3) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Sura ya 123. Kifungu cha 87(1) kinarekebisheswa ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwa malighafi za

mbolea inayochimbwa hapa nchini kutoka asilimia tatu hadi asilimia moja, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, imeishauri Serikali hatua hii iwe ni ya mwaka mmoja ili kuangalia endapo inatimiza malengo yaliyokusudiwa. Aidha, kwa kuwa sekta ya mbolea imepata msamaha kwenye kodi ya ongezeko la thamani kwa kutozwa kwa kiwango cha asilimia sifuri na pili kupunguziwa mrabaha ni vyema sasa Serikali ikaweka utaratibu wa kupanga bei elekezi kwa mbolea inayozalishwa ndani ili kuhakikisha kwamba, mbolea hii inamfikia mkulima kwa bei nafuu. Endapo suala la bei litaachiwa kwa wamiliki wa viwanda ni wazi kwamba, manufaa hayatamfikia mkulima na badala yake wazalishaji watajietengenezea faida ya kupindukia (*super normal profit*).

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuongeza madini ya chokaa yanayotumika kwa ajili ya kuzalishia mbolea nayo kutozwa mrabaha wa asilimia mouja ili pia viwanda vinavyotumia madini hayo navyo kunufaika na pungozo hilo. Lengo la msingi ni kuongeza uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi na kupunguza bei kwa wakulima.

(4) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Barabara. Kifungu cha 8 kinarekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe ushuru wa mafuta kwa miradi ya uwekezaji mahiri na mahiri maalum itakayoidhinishwa na Kamati ya NISC. Uzoefu unaonesha kwamba, kama kuna moja ya msamaha ambao umetumika vibaya ni msamaha wa ushuru wa mafuta, hivyo, kutokana na uzoefu huo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

- (i) Kuwepo na muda maalum wa kusamehe ushuru kwenye mafuta baada ya mradi kukamilika;
- (ii) Kwa kuwa mfumo wa kuagiza mafuta ni wa pamoja, lazima kuwe na namna ama ya kutofautisha kwa vinasaba au uuzaji wake ili kuondoa mwanya wa matumizi mabaya;
- (iii) Kuweka mfumo wa usimamizi ili kuzuia mafuta yaliyokuwa yatumike kwa ajili ya miradi kutumika katika shughuli tofauti; na
- (iv) Inashauriwa pia kwamba, sharti la kuondoa msamaha lililopo katika Kanuni za Sheria hii lilekelezwe endapo itaonekana msamaha umetumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu wa Kamati ni kuhakikisha kwamba, msamaha huu usije ukasababisha uuzaji holela wa mafuta hapa nchini (*dumping*). Aidha, Kamati iliishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti la kwamba, endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo haijokusudiwa, msamaha huo utaondolewa na mhusika atalazimika kulipa ushuru stahiki. Marekebisho hayo yanaonekana kuititia Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

(5) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT); Kifungu cha 6 kinafanyiwa marekebisho ili kujumuisha uwekezaji mahiri ulioihinishwa na Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji ambapo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, kuongeza Kifungu kipyaa cha 55A kwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwa mbolea inayozalishwa ndani ya nchi ili kuleta unafuu kwa wakulima na watumiaji wa mbolea. Vilevile kurekebisha Jedwali ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa magunia ya mkonge yanayotengenezwa hapa nchini yanayotambulika kwa HS Code 6505.90.00 na malighafi inayotambulika chini ya HS Code 72299000 ambayo hutumika kutengenezea mitungi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubalina na Serikali kwa mabadiliko katika sheria hii kwa lengo la kupunguza bei ya magunia yanayozalishwa ndani. Hata hivyo, iliishauri Serikali na Serikali ikakubali kuweka ukomo wa mwaka mmoja ili kuangalia endapo msamaha huo unaleta manufaa yanayokusudiwa. Aidha, Kamati ilishauri kwamba, kuhusu msamaha wa malighafi za kuzalisha mitungi ya gesi usitolewe katika kipindi hiki kwa sababu, utaathiri mapato ya Serikali. Serikali ilikubali pendekemo hilo la Kamati na Ibara ya 15B ya Muswada iliondolewa, kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Jumla; masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kuitisha Muswada wa Sheria ya Fedha ni kama yafuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, kufanya tathmini na utafiti wa faida na hasara ya misamaha ya kodi ambayo inatolewa na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inajiridhisha na misamaha ya kodi pamoja na vivutio vingine vinavyolenga kuvutia wawekezaji nchini. Kujiridhisha kwa hatua hizo ni kuhakikisha kuwa inaleta matokeo tarajiwa na sio kuipotezea Serikali mapato. Aidha, kuwepo na usimamizi mzuri wa misamaha inayotolewa na Serikali kwa wawekezaji mahiri pamoja na wa kimkakati.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwa Pato la Taifa (*Tax Exemption against GDP*). Misamaha ya kodi ni hatua ya sera za mapato ambayo huwa na malengo mbalimbali kama vile kuchochea uzalishaji, kupunguza gharama za huduma au bidhaa, kugawanya rasilimali na kuchochea ukuaji wa sekta. Hata hivyo, malengo tuliojiwekea katika Mpango wa Miaka Mitano, misamaha haitakiwi kuzidi asilimia Moja ya Pato la Taifa, hivyo ni wakati sasa kwa Serikali kufanya tathmini ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuona endapo misamaha hiyo imefikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuimarisha vitengo vya utafiti kwa sera za mapato ili kuiwezesha Serikali kuwa na taarifa za uhakika pindi inapoandaa Sera za mapato. Kuna haja ya msingi ya kuimarisha vitengo vya utafiti wa sera za mapato na hasa kodi kwa kuvitengea rasilimali watu na fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini mabadiliko yanayofanywa mara kwa mara katika sheria za kodi ni kutokana na kutokuwa na utafiti wa kutosha wa kina katika sera za mapato.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha Na. 13 wa Mwaka 2022 mbele ya Bunge lako tukufu.

Pili, nimshukuru Mheshimiwa Mussa Azan Zungu Mbunge Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Mbunge, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hassan Chande Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hussein Bashe Mbunge Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Exaud Kigahe Mbunge, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi wa Sheria wa Bunge kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao uliowezesha Kamati kuchambua Muswada huu hadi kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omar Kigua, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, vilevile napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umakini, umahiri na uvumilivu wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Naomba orodha yao ya majina ya Wajumbe hao yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi Nenelwa Mwihambi - ndc, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndugu Michael Kadebe ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofii)

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA  
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI ZA FEDHA NAMBA 13 WA MWAKA 2022  
[THE WRITTEN LAWS (FINANCIAL PROVISIONS) (AMENDMENTS) BILL, 2022] –  
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha Namba 13 wa Mwaka 2022 **The Written Laws (Financial Provisions) (Amendment) Act, 2022**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 19 Septemba, 2022, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha na 13 na baada ya kuwasilisha Muswada huo, Mheshimiwa Spika uliiagiza Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuuchambua muswada huo ili baadaye maoni yake yawasilishwe Bungeni.

**1.1. Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa muswada huu kwa kupitia kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujelimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, tarehe 19 hadi 21 Septemba, 2022 Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Kilimo; Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, pamoja na Watendaji wa Wizara. Aidha, Kamati pia ilikutana na wadau kwa ajili ya kupokea mapendekezo na maoni yao juu ya marekebisho yanayopendekezwa. Wadau waliofika kwenye Kamati ni Aliko Vintage.

**2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu una madhumuni makubwa matatu kama ifuatavyo: -

- i. Kuchochea uzalishaji wa mbolea nchini ili zipatikane kwa bei nafuu;
- ii. Kutoa vivutio maalumu kwa miradi ya kimkakati na mahiri ili kuchochea uwekezaji kwenye miradi mikubwa yenyе kuleta mapinduzi ya kiuchumi; na

iii. Kuchochaea uzalishaji ndani hasa wa bidhaa za magunia na mvinyo ili kuchochaea kilimo cha mazao ya zabibu na katani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutazama madhumuni haya ya muswada nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hasan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonyesha nia ya dhati ya kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mikubwa inayoleta mapinduzi ya kiuchumi. Kamati inaamini kwa masharti yaliyoko kwenye muswada huu Mhe Rais atakuwa ameonyesha kwa vitendo namna bora ya kutanzua vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

### **3.0. MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI ZA FEDHA NAMBA 13 WA MWAKA 2022.**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria tano za Kodi ambazo ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, Sheria ya Madini Sura ya 123, Sheria ya Ushuru wa Mafuta 220 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sura ya 148. Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

#### **3.1. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 (The Excise Management and Tariff) Act, Ca147)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kurekebisha kifungu cha 128 ili kumpa Mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, baada ya kupata idhini ya Baraza la Mawaziri kusamehe ushuru kwenye bidhaa zitakazotumika katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji mahiri na ya kimkakati itakayoidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (NISC) pamoja na kupandisha ushuru wa Bidhaa za mvinyo kutoka nje kutoka **shilingi 2,466.45** hadi **shilingi 5,600** kwa lita ili kulinda wakulima wa ndani wa zao la zabibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa nchi za jirani zinatoza kati ya **shilingi 5,000** hadi **5,500** kwa lita ya mvinyo unaotoka nje, hivyo hatua hii inahuisha viwango vinavyotozwa katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki. Aidha, hatua hii inaleta usawa wa kiushindani kati ya wazalishaji wa zao la zabibu nchini dhidi ya mataifa mengine ambayo yameendelea sana katika uzalishaji wa zao hili. Hivyo, Kamati inakubaliana na pendekeso hili ambalo lina nia njema la kusaidia na kuinua viwanda vya ndani na kuwa shindani. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ubora wa mvinyo unaozalishwa ndani ya nchi pamoja na kuchochaea kilimo cha aina mbalimbali za zabibu ili kuhakikisha kwamba malighafi hii muhimu kwa utengenezaji wa mvinyo inapatikana ndani ya nchi. Aidha, Kamati ilishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti kwamba, endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo haijakusudiwa, msamaha huo utaondolewa

na muhusika atalazimika kulipa ushuru stahiki. Marekebisho hayo yanaonekana kuitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### 3.2. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 (*The Income Tax Act, (Cap 332)*)

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kujumuisha uwekezaji mahiri uliodhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji- NISC, katika wigo wa maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana ya Masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya mapato. Aidha, mapendelekezo haya yanabainisha kwamba misamaha ya kodi ya mapato itakayokuwa inatolewa kuitia mikataba ambayo Serikali inaingia na wawekezaji ndio itatumika wakati wa kukokotoa Kodi ya Mapato.

**Mheshimiwa Spika**, hatua hii ina nia njema ya kutanzua mkwamo wa Miradi ya Kimkakati ya wawekezaji mahiri. Uzoefu unaonyesha kuwa kuna baadhi ya wawekezaji mahiri wametumia mikataba yao vibaya kuhakikisha kwamba Serikali haipati mapato yake inayostahili. Aidha, Kamati ilishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti la kwamba endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo haijokusudiwa, msamaha huo utaondolewa. Marekebisho hayo yanaonekana kuitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### 3.3. Sheria ya Madini Sura, Sura 123 (*The Mining Act, (Cap 123)*)

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 87 (1) kinarekebishwa ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwa malighafi za mbolea zinazochimbwa hapa nchini, kutoka **asilimia 3** hadi **asilimia 1**. Kamati imekubaliana na mapendelekezo ya Serikali. Hata hivyo, imeishauri Serikali hatua hii iwe ni ya mwaka mmoja ili kuangalia endapo inatimiza malengo yaliyokusudiwa. Aidha, kwa kuwa sekta ya mbolea imepata msamaha kwenye kodi ya ongezeko la thamani kwa kutozwa kwa asilimia sifuri na pili kupunguziwa mrabaha ni vyema sasa Serikali ikaweka utaratibu wa kupanga bei elekezi kwa mbolea inayozalishwa ndani ili kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima kwa bei nafuu. Endapo suala la bei litaachiwa kwa wamiliki wa viwanda ni wazi kwamba manufaa haya hayatamfikia mkulima na badala yake wazalishaji watajitengenezea faida ya kupindukia (super normal profit).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri Serikali na ikakubali kuongeza madini ya chokaa yanayotumika kwa ajili ya kuzalisha mbolea nayo kutozwa mrabaha kwa **asilimia 1** ili pia viwanda vinavyotumia madini hayo navyo kunufaika na punguze hilo. Lengo la msingi ikiwa ni kuongeza uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi na kupunguza bei kwa wakulima.

**3.4. Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Barabara (The road Fuel Toll Act, (Cap 220)**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 8 kinarekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe ushuru wa mafuta kwa miradi ya uwekezaji mahiri na mahiri maalum itakayoidhinishwa na Kamati ya NISC. Uzoefu unaonyesha kwamba kama kuna moja ya msamaha ambao umetumika vibaya ni msamaha wa ushuru wa mafuta. Hivyo, kutokana na uzoefu huo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

- i. Kuwepo na muda maalumu wa kusamehe ushuru kwenye mafuta baada ya mradi kukamilika;
- ii. Kwa kuwa mfumo wa kuagiza mafuta ni wa pamoja lazima kuwe na namna ama ya kutofautisha kwa vinasaba au uuzaji wake ili kuondoa mwanya wa matumizi mabaya;
- iii. Kuweka mfumo wa usimamizi ili kuzuia mafuta yaliyokuwa yatumike kwa ajili ya miradi kutumika katika shughuli tofauti;
- iv. Inashauriwa pia kwamba sharti la kuondoa msamaha lililopo katika kanuni za Sheria hii litekelezwe endapo itaonekana msamaha umetumika vibaya.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri huu wa kamati ni kuhakikisha kwamba msamaha huu usije ukasababisha uuzaji holela wa mafuta nchini (dumping). Aidha, kamati ilishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti la kwamba endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo haijokusudiwa, msamaha huo utaondolewa na muhusika atalazimika kulipa ushuru stahiki. Marekebisheso hayo yanaonekana kupitia jedwali la marekebisheso la Serikali.

**3.5. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (Value Added Act, (Cap 148)**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 kinafanyiwa marekebisheso ili kujumuisha uwekezaji mahiri ulioidhinishwa na Kamati ya NISC, ambapo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, kuongeza kifungu kipy cha 55A kwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha 0 kwa mbolea inayozalishwa ndani ya nchi ili kuleta unafuu kwa wakulima na watumiaji wa mbolea. Vilevile, kurekebisha jedwali ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa magunia ya mkonge yanayotengenezwa nchini inayotambulika kwa HS Code 6305.90.00 na malighafi inayotambulika chini ya HS Code 7229.90.00 ambayo hutumika kutengeneza mitungi ya gesi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na Serikali kwa mabadiliko katika sheria hii kwa lengo la kupunguza bei ya magunia yanayozalishwa ndani. Hata hivyo, ilishauri Serikali na ikakubali kuweka ukomo wa mwaka mmoja ili kuangalia endapo msamaha huo unaleta manufaa yaliyokusudiwa. Aidha,

Kamati ilishauri kwamba kuhusu msamaha wa malighafi za kuzalisha mitungi ya gesi usitolewe katika kipindi hiki kwa sababu unaathiri mapato ya Serikali. Serikali ilikubali pendekezo hilo la Kamati na ibara ya 15 (b) ya muswada iliondolewa kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

#### **4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika**, masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha ni kama ifuatavyo: -

##### **4.1. Kufanya tathmini na Utafiti ya Faida na Hasara ya Misamaha ya Kodi ambayo inatolewa na Serikali.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishuri Serikali kuhakikisha kuwa inajiridhisha na misamaha ya kodi pamoja vivutio vingine vinavyolenga kuvutia uwekezaji nchini. Kujiridhisha kwa hatua hizo ili kuhakikisha kuwa inaleta matokeo tarajiwa na sio kuipotezea Serikali mapato. Aidha, kuwepo na usimamizi mzuri wa misamaha inayotolewa na Serikali kwa wawekezaji mahiri pamoja na wa Kimkakati.

##### **4.2. Misamaha ya Kodi kwa Pato la Taifa (Tax exemption/GDP)**

**Mheshimiwa Spika**, Misamaha ya Kodi ni hatua ya Sera za Mapato ambayo huwa na malengo mbalimbali kama vile kuchochea uzalishaji, kupunguza gharama za huduma au bidhaa, kugawanya rasilimali na kuchochea ukuaji wa sekta. Hata hivyo malengo tuliojiwekea katika Mpango wa Miaka mitano misamaha haitakiwi kuzidi asilimia 1 ya pato la Taifa. Hivyo ni wakati sasa kwa Serikali kufanya Tathmini ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuona endapo misamaha hiyo imefikia malengo yaliyokusudiwa.

##### **4.3. Serikali kuimarisha Vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato ili kuiwezesha Serikali kuwa na Taarifa za uhakika pindi inapoandaa sera za mapato.**

**Mheshimiwa Spika**, Kuna haja ya msingi ya kuimarisha vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato na hasa kodi kwa kuvitengea rasilimali watu na fedha za kutosha ili vitekeleze majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini mabadiliko yanayofanywa mara kwa mara katika sheria za Kodi ni kutokana na kutokuwa na utafiti wa kina katika sera za mapato.

#### **5.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha Na 13 wa Mwaka 2022

mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nimshukuru Mhe Mussa Azzan Zungu, Mb - Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha napenda nimshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hussen Bashe Waziri wa Kilimo, Mhe. Exaud Kigahe Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Muandishi wa Sheria wa Bunge kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda Kumshukuru Mhe. Omari Kigua Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na vilevile napenda kuwashukuru Wajumbe wa kamati ya Bajeti kwa umakini, umahiri na uvumilivu wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu, hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Wajumbe hao ni:

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Dkt Charles Kimei, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Mariam Kisangi, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi ndc pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za

Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

22 Septemba, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana MwenyeKITI wa Kamati ya Bajeti kwa kutupa mwelekeo wa namna Kamati iliyofanyakazi kwenye Muswada huu. Waheshimiwa Wabunge ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii, tutaanza na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Jonas Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye huu Muswada. Jambo la kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuja na mapendekezo ambayo yatakwenda kusaidia sana kuboresha maeneo ambayo kweli yalikuwa na matatizo. Hizi Sheria Tano zinazorekebishwa yale maeneo yanayorekebishwa yalikuwa yanaleta matatizo ya kuchelewesha hasa baadhi ya miradi na kuchelewesha uwekezaji na kuathiri hasa hasa eneo la wakulima.

Mheshimiwa Spika, tunayo miradi mikubwa ya kimkakati ya uwekezaji mahiri imechelewa kwa muda mrefu, mradi kama Liganga na Mchuchuma na miradi mingine ya aina hiyo, kama hii miradi ambayo tunaendelea kuzungumza kuhusu ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ina elements kama hizo. Nahisi kwamba sheria hii marekebisho haya hasa kwenye eneo hilo yamechelewa sana na yametuchelewesha kweli kupata faida kubwa kutokana na uwekezaji kwenye miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria ya uwekezaji nzuri, imeweka utaratibu mzuri, tunakwenda kwenye Baraza la Ushauri la Uwekezaji chini ya Waziri Mkuu mwenyewe kabisa na Mawaziri ni Wajumbe, lakini wakitoa maamuzi au ushauri au mapendekezo, Waziri wa Fedha alikuwa anakosa power ya kuweza kutekeleza mapendekezo ambayo yametoka kwenye Baraza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo marekebisho ambayo yanakuja kuitia marekebisho haya, yanakwenda kumpa nguvu sasa Waziri wa Fedha baada ya approval ya Baraza ili aweze kutekeleza mapendekezo ya Baraza la Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, napenda kuwashawishi wenzangu kwamba tukubali, Bunge likubali marekebisho haya ili kuweza

kuisaidia nchi kutekeleza miradi mikubwa ambayo inayo faida kubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza sana kile kipengele ambacho kimewekwa cha kuweka angalizo ili hawa watakaopewa misamaha wasiitumie vibaya, napenda kuiomba Serikali iwe macho ili hawa ndugu zetu ambaa watakuwa wamepewa misamaha basi waitumie vizuri misamaha hiyo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kumekuwa na kilio cha siku nyingi sana kuhusiana na togwa la zabibu au wengine wanaita mchuzi tulikuwa tunabishana ni mchuzi au togwa? Mimi nadhani mchuzi ni ule wa nyama sasa hii kuita mchuzi wa zabibu kidogo ilikuwa inaleta shida. Kwa hiyo, mimi napenda kutumia neno togwa la zabibu.

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi wa Dodoma hapa walikuwa wanalamika sana kwamba wanakosa soko na mambo kama hayo. Kwa hiyo, hii hatua inayo pendekenzwa hapa ya kuongeza kodi kwenye uagizaji wa nje wa bidhaa hizi za togwa la zabibu na wines ni hatua ambayo itasaidia wakulima wetu wapate soko. Kwa hiyo, ni jambo ambalo sasa na Wagogo nao wataanza kupata uchumi kutoka kwenye kilimo, akina Mheshimiwa Simbachawene hawa. Kwa hiyo, wenzetu hapa sasa Wagogo wataanza kuongeza uzalishaji kwa sababu sasa watakuwa na soko la uhakika, hii ni hatua ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo ningependa nilizungumzie kutokana na marekebisho haya ni eneo la mbolea. Tangu tulipopata janga la UVICO-19 viwanda vilifungwa duniani, karibu viwanda 6,000 vilifungwa duniani vya kuzalisha mbolea, kukawa na uhaba mkubwa sana wa mbolea, sasa kwa sababu sisi hatuna kiwanda cha mbolea ndani ya nchi tunategemea kuagiza nje gharama za usafirishaji na ununuzi zilipandisha bei ya mbolea kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo hatua hapa ambayo kwanza naanza kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo imechukua mwaka huu ya kuweka ruzuku kwenye mbolea ambayo imeshusha bei ya mbolea ni hatua muhimu sana hongera sana Mheshimiwa Rais, hongera sana Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha hiyo ni hatua muhimu sana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua ambayo sasa inakuja ku-target kupunguza gharama za uzalishaji kwa kupunguza mrabaha kutoka asilimia. Tatu hadi asilimia Moja kwenye enforcement ambayo ni malighafi muhimu kwenye utengenezaji wa mbolea, hii ni jambo ambalo ni muhimu sana na kwa kweli limekuja katika wakati muafaka kwa nchi hii ambapo sasa tunaenda kuwa na kiwanda kitakachozalisha tani Laki Sita za mbolea hapa hapa Dodoma na tuna kiwanda kingine kule Manyara cha Minjingu kinazalisha nadhani karibu tani Elfu Thelathini sina takwimu sahihi. Kwa hiyo, ina maana kwamba katika muda mfupi ujao kupitia kipengele hiki tutaenda

kushusha gharama za mbolea inayozalishwa nchini. Kwa hiyo, hii nayo ni hatua ambayo kwa kweli ni ya kupongeza sana Serikali na tukipitisha humu haya marekebisho ya sheria basi tunaenda kumsaidia mkulima wa nchi hii aweze kupata mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa gharama nafuu. (makofi)

Pili, ninaipongeza Serikali imekuwa sikivu sana kwenye majadiliano hasa hasa mwanzoni tulipokuwa tunapendekeza kwamba madini ya chokaa nayo ni muhimu sana katika utengenezaji wa mbolea. Kulikuwa na debate kubwa kulikuwa na mazungumzo mrefu kwamba sasa tutadhiliti namna gani kwa sababu chokaa inayo matumizi mengi kwenye viwanda, kwenye ujenzi na kwenye maeneo mengine. Chokaa yenye ukiwaga kwenye ardhi inaongeza rutuba kwenye ardhi, chokaa yenye chokaa yenye ni mbolea vilevile chokaa yenye ni malighafi katika kutengeneza mbolea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii hatua ya kukubali chokaa nayo iingizwe isipokuwa waongeze tu usimamizi na udhibiti ni jambo la kuipongeza sana Serikali, naomba sana Bunge lako Tukufu likubali marekebisho haya ili kumsaidia Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba sana niseme kwamba naunga hoja mkono. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jonas Mbunda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kime, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Fedha pamoa na jopo lake kwa kuleta mabadiliko ya sheria hizi ambazo moja kwa moja sehemu kubwa zinalenga kuwasaidia wakulima wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutenga kiasi cha Shilingi Bilioni 150 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbolea, hilo ni suala la muhimu sana na limeleta faraja kubwa sana kwa wakulima wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitachangia Miswada hii hasa kwenye maeneo ambayo yanagusa wakulima. Eneo la kwanza Serikali imeleta mapendeleko ya kubadilisha Muswada wa Sheria Sura Na. 123 Kipengele cha 87(1) ambacho kimependekeza kupunguza mirahaba ya ushuru kwenye malighafi mbalimbali ambazo zinatumika kwa ajili ya kutengeneza mbolea. Suala hilo ni la muhimu sana, jambo la kwanza ni lilelile eneo sikivu la Serikali la

kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanufaika na kilimo katika nchi yetu. Suala la pili ni jambo la msingi ambalo litavutia wawekezaji wa viwanda mbalimbali vya mbolea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili la kupunguza mirabaha kutoka asilimia Tatu mpaka Moja ni suala la msingi sana, kwa sababu litasaidia kupunguza ghamama mbalimbali za uzalishaji wa mbolea, kama mlivyoona kwamba kwa mwaka huo uliopita ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakulima, kwa hiyo tunaona kabisa wazo hili la Serikali litasaidia kuleta manufaa makubwa sana kwa wananchi katika nchi hii. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii ya Serikali naomba nitoe ushauri ufuatao: Ushauri wa kwanza, naionba Serikali sasa kama Wabunge wenzangu wataunga mkono na tukapitisha sheria hii, Serikali iweze kusimamia kwa karibu sana ili tuweze kupata matokeo chanya na tuone kabisa punguzo hili limewasadida wakulima. Ushauri mwingine kama patakuwa na uwezekano Serikali iangalie uwezekano wa kutoa bei elekezi za mbolea kwa wakulima wetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo tungeomba yahusishe madini yote ambayo yatatumika kwa ajili ya kutengeneza mbolea. Kwa maelekezo ambayo yametolewa kupitia Muswada huu kwenye upande wa phosphate vilevile chokaa ambayo itasaidia sana kurekebisha hali ya udongo katika maeneo mbalimbali ili wakulima waweze kutumia kiasi cha mbolea kidogo sana baada ya udongo kurekebishwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali hoja yangu italenga hasa hasa kwa maeneo ambayo yanamnufaisha mkulima.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni kwenye suala la ushuru wa ongezeko la thamani. Wakulima wa mazao mbalimbali ukichukulia mfano wa zao la kahawa, korosho na mazao mengine kwa muda mrefu walikuwa wakilipa ghamama kubwa sana ya magunia katika kuhifadhi hayo mazao mbalimbali na ghamama hizo zinatokana na ghamama kubwa ya uzalishaji wa hayo magunia ya katani.

Mheshimiwa Spika, tunavyo viwanda zaidi ya kimoja ambavyo vinazalisha magunia ya katani lakini wakulima walikuwa wanalipa bei kubwa sana kwa gunia moja la kuwekea kahawa au korosho kutokana na ghamama kubwa ya uzalishaji. Kwa hiyo, hii Sheria Sura Na. 148, ambayo Serikali itatoa unafuu itatoa exemption kwenye uzalishaji wa haya magunia itasaidia sana kupunguza bei kubwa ya magunia na itapelekea kuwapa unafuu wakulima wetu kuweza kupata kipato kikubwa kwa sababu bei ya gunia moja ambalo watakuwa wanatumia kuwekea mazao haya itakuwa imepungua. Hiyo nayo itaendelea kuleta faraja kwa wakulima na itaendelea kuleta hamasa

kubwa sana ya wakulima kuona kwamba mazao ambayo wanalima yanawasaidia kwenye masuala ya maisha.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho naomba nichangie kwenye jedwali la Nne linalohusu mapendekezo ya Serikali ya kuongeza ushuru wa mvinyo kutoka Shilingi 2,466.45 kwa lita hadi Shilingi 5,600 kwa lita. Hiyo itasaidia sana kupunguza bidhaa zinazotokana na mvinyo kuingia nchini na itasaidia sana kulinda soko la wakulima wa zao hili la zabibu ili kuweza kuwapa hamasa kubwa zaidi ya kuendelea kujali kilimo chao na kuwafanya waridhike na hali halisi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo naomba niishauri Serikali kuzingatia mambo yafuatayo:-

Kwanza; Serikali isimamie sasa ubora wa uzalishaji wa mvinyo ambao tunazalisha ndani ya nchi ili kuhakikisha kwamba tunaingia kwenye ushindani kwenye soko la mvinyo;

Pili; Baada ya kuitisha sheria hii Serikali iangalie kama mvinyo unaozalisha nchini utaweza kutosheleza mahitaji ya viwanda vyetu vinavyozalisha bidhaa za mvinyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naomba niunge hoja kwa Miswada hii. Ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii na nianze pia kwa kuijunga na wenzangu kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu anayeongoza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuanza kuchukua hatua madhubuti na za kimkakati za kuongeza uwekezaji na kasi ya uwekezaji katika uchumi wetu, kwa vile mimi naona kwamba Muswada huu una maudhui ya kimkakati kabisa na siyo tu kwamba, tunaona kwamba kuna kupunguza hapa na pale lakini utaona kwamba ni Muswada au ni marekebisho ambayo yanaenda kumpa Mheshimiwa Waziri wa Fedha uwezo wa kufanya maamuzi ya haraka ili kuweza kuruhusu miradi ile mahiri na ya kimkakati kuanza hapa nchini upesi bila kusubiri bureaucracy ya kupeleka kwenye Bunge kwa sababu sheria za kikodi mara nyingi zinahitaji zirudi huku Bungeni, na naamini kwamba Mheshimiwa Rais ameruhusu Muswada huu uje ili uweze kufupisha ule mchakato wa Mwekezaji kuweza kufika na kuanza mradi wake.(Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tunaofahamu ni kwamba, Wawekezaji wote na miradi mingi inakuwa na mahitaji tofauti tofauti ili iweze kuonesha

kwamba itakuwa na faida katika kipindi ambacho yule Mwekezaji amejiwekea. Bila yale masharti au zile athari ambazo yeye anaziona kwenye mradi ule, hazijawa addressed kwa namna ambapo yeye na Bodi zake, kama ziko nje ya nchi au ziko hapa hapa nchini, basi inakuwa vigumu sana kuchukua hatua ile ya kuanza kutekeleza mradi.

Mheshimiwa Spika, mara nyigi watapita kwenye maeneo mbalimbali, wataanza *TIC* ambapo baadaye wataishia hata kwenye *National Investment Steering Council* - Kamati ya Uwekezaji ya Taifa, lakini kama hawana uhakika kwamba yale wanayojadili, yale yanayojadiliwa na taasisi hizi hayatatekelezwa haraka, ni lazima pengine yaje Bungeni yaulizwe maswali mengi, pengine yasipite, basi inakuwa ni vigumu sana miradi ile kuanza.

Mheshimiwa Spika, nami naamini kwamba hili mkakati wake unatokana hilo; kwamba sasa Waziri wa Fedha, na niseme kwamba sio tu Waziri wa Fedha; na tumeridhika sana kule kwenye Kamati yetu kuona kwamba Waziri wa Fedha atatekeleza haya baada pia ya kupitia kwenye cabinet kwenye maeneo fulani fulani; lakini ni miradi ile ambayo imepita kwenye Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ambayo inasimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Siyo tu Waziri Mkuu, pia ndani yake kuna kuna watu ambao ni mahiri, ni watu ambao ni wazalendo ambao tunajua kwamba wanaongoza taasisi ambao zinaelewa masuala ya uwekezaji kwa mapana kama vile Benki Kuu na wengine. Kwa hiyo ninaamini tutakwenda mbali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunajua kabisa kwamba, tena tumeambiwa, kuna congress man mmoja kule Marekani ambaye ame-trend sana; natumaini wengi wameona; anatoa changamoto. Kwamba ukweli tatizo kubwa la uwekezaji huku nchini linatokana na kodi nyigi na kubwa. Ile corporate tax, ukienda kwenye VAT ziko juu. Na nini, mimi ninakubaliana naye kwa namna fulani. Ni kweli kwamba tusipoangalia vizuri na tusipoweza ku-treat kila mwekezaji kwa namna fulani ambayo inampa au kinampa uhakika; kwamba zile ghamra zisipoweza kupunguzwa, zikafanywa hivi kwa kupunguza VAT kwa muda fulani tutakaa muda mrefu bila kuona uwekezaji ukiongezeka. (Makof)

Mheshimiwa Spika, na huu uwekezaji unashindaniwa. Kila nchi inashindania uwekezaji kwasababu inajulikana kwamba capital discuss duniani ni taji, haipo tu hovyo hovyo, ni taji inashindaniwa na nchi mbalimbali na shughuli mbalimbali, na kila nchi inajaribu kutoa kwa namna fulani vivutio ambavyo vinaweza kuwezesha wawekezaji wakaingia. Kuna nchi nyininge sasa hivi zimeanza, na natumaini ni nadharia mpya ambayo inakuja; kwamba *the only way* ya kuongeza tax base ili kuongeza government revenue bila kuongeza viwango vya kodi ni kuongeza uzalishaji. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa, kama hatuwezi kuongeza uzalishaji kwa namna hii ya kuvutia wawekezaji, kitu ambacho hatuna uzalishaji ambao haupo lakini tukiwavutia watakuja tukawapa *dispensations* fulani, tukawapa misamaha fulani kwa kipindi ambacho kinakubalika hawa wawekezaji wakaja wakaongeza uzalishaji tukaanza kuvuna *Pay as You Earn*, tukaanza kuvuna vyote vile vingine vinavyotokana na uzalishaji kuongezeka katika nchi hii hakutafika mbali. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwasababu naona kwamba hii nadharia ameweza kuiona. Kwamba njia pekee sasa ya kuweza kuongeza *taxbase* yake si tu kuchukua from kilichopo lakini tuongeze uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, na hata tusipowakaribisha kwa kuwapa hizi *dispensations* wanazoomba hatutakuwa nao, uzalishaji hautakuwepo; lakini tukifanya vile kwa muda mfupi watakuwepo, tutaona uzalishaji utaongezeka na *taxbase* yetu itakuwa ina-grow na itakuwa inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwamba Muswada huu umebuniwa vizuri. Kwa mfano tumeona kuna vingi vinalenga mwenye kiwanda hiki cha kuzalisha mbolea, utaona kila mtaji ukija utakuwa hivyo hivyo, utakuwa na vitu vingine vinahitajika, si kupunguza tu bei ya phosphate au kutoa mrhaba kwenye phosphate, mwagine atakuja na ombi lingine kutokana na jinsi ambavyo anawekeza. Kwa hiyo ni vizuri tukampa Waziri wa fedha na pia tukahakikishiwa kwamba kwa vile hivi vitu sio yeye anafanya mwenyewe, vitaenda hadi kwenye Cabinet ambayo Mheshimiwa Rais mwenyewe atakuwepo; hivyo haiwezi kuwa abuse. Mimi ninaamini kwamba tutakwenda vizuri, na hiyo ndiyo inaonesha wazi kwamba miradi mingine ili iweze kwenda fast na iweze kutekelezwa kwa kipindi kifupi ni lazima tutoe uwezo kwa Serikali kuweza kufanya hayo mambo bila kupoteza muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninachelea kusema kwamba naungana na Kamati na nilikuwepo, na ninashukuru kwamba Kamati imeshauri pia kwamba kwa baadhi ya misamaha inayotolewa iwe inachapishwa na Serikali kwenye gazeti ili watu wajue, kwamba katika kipindi hiki Serikali imetoea misamaha hii na watu wataona mahudhui kwasababu gani misamaha hiyo imetolewa na hakuna mtu atalalamika kwamba kuna misamaha ambayo imetoka kienyeji enyeji. Kwa hiyo ninaamini ikichapishwa itakuwa imesaidia, lakini pia ni *transparency* na ndio dhana zima ya uendeshaji wa Serikali (*good governance*) sasa hivi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, halafu pia ninaamini kwamba huo ushauri ambao umetolewa, kwamba Serikali iwe inafanya tafiti za mara kwa mara, kufanya tathmini ya ile misamaha iliyotolewa au zile punguzo zilizotolewa kwenye maeneo fulani fulani ya kodi kama ni VAT whatever kwamba imeleta matokeo chanya yanayoendana na mahudhui ya marekebisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshauri pia kwamba kuwe na *timeframe* ya hiyo ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa malizia.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ... *time flame* iwepo. Kwamba wakati unapotoa ile misamaha ijulikane inaisha ndani ya utekelezaji wa mradi na pia ndani ya muda mfupi baada ya mradi kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa fursa hiyo, nataka niseme kwamba naunga mkono hoja iliyiletwa na Mheshimiwa Waziri ya kurekebisha hizi sheria lakini pia naomba Wabunge wenzangu waweze kona maudhui haya kwa u-chanya wake ili waweze kupitisha hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwanza kwa kutupa uhai na cha pili kutujalia tukaja hapa tukiwa wazima, na kitu kingine nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze na pongezi kwa Serikali kwanza kwa kuleta Muswada huu, lakini cha pili niishukuru Serikali kwa kukubali ushauri na kutengeneza *schedule of amendments* baada ya kupata ushauri wa Kamati katika masuala ambayo yameletwa mbele ya Kamati. Pia naunga mkono hoja zote ambazo zimewasilishwa na Kamati ya Bajeti ambazo zime lenga kuishauri Serikali katika maeneo mbalimbali katika Muswada huu ambao umeletwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kiufupi Muswada huu ulikuwa una Sheria nne ambazo zinakwenda kubadilishwa ili ziende sanjari na ile sheria tulioipitisha, ambayo inahusiana na *strategic investment*, ambayo inakwenda sambamba kwenda kurekebisha sheria ya *excise duty, road and fuel tolls* sheria ya *cooperate tax* na VAT kwa ajili ya Kwenda sanjari ili kufanya uwekezaji wa kimkakati uweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na hayo ninaushauri ufuatao; ushauri wangu wa kwanza, kwenye punguzo ambalo tumetoa, kuna sheria zime lenga kwenye kupunguza, kwa mfano kuna sheria ina punguza royalty, kuna sheria pia inaweka zero rate, lakini pia kuna pendekero la sheria hapa ya VAT ya kuweka exemption. Kwa hiyo sheria hizi ambazo zitapunguza mimi nilikuwa nataka kusema msemo mmoja. Tunasema aliyeumwa na nyoka

akiona unyasi anashtuka, sasa tumewahi kuwa na sheria ambazo tunatoa punguzo, tumewahi kuwa na sheria ambazo tunaweka zero rate na tumewahi kubadilisha sheria tukaweka exemption kwa ajili ya kuwapa nafuu watumiaji ambao ni wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hiyo baada ya kupitishwa ikifika kwenye kutumika hatuoni ule unafuu unaopatikana. Ninajaribu kutoa mfano wa sheria hizo; tuliweka hapa zero rate kwenye simu zitakazoingizwa (smartphones) na kwenye sanitary pads lakini baadaye hatukuona bei iliyopungua wala unafuu ambao umepatikana. Kwa hiyo niishauri Serikali, kwenye kulifanya kazi hili Serikali *at least* iweke mikataba na watu hawa. Wasipokuja na solution ile ambayo tumeikusudia ina maana kwamba lengo la utungaji au kubadilisha sheria hizi hatuwezi kuufikia. Kwa hiyo niwaambie Serikali kwamba tujaribu kuweka measures ambazo zitadhibitisha na kupata ule unafuu tulioulenga, vinginevyo ndio tutaona huyu ndiye nyoka yule yule. kwa hiyo sasa hivi tunaona unyasi hapa atakuja kutugonga tena.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie upunguzaji au kusamehe exercise duty kwaajili ya miradi ya kimkakati. Ni kweli tumepanga bidhaa zitakazoingizwa nchini kwaajili ya miradi ya kimkakati tutoe huo msamaha. Sasa, niishauri Serikali kwamba kabla ya kupitisha kwasababu humu ndani tuna viwanda ambavyo vinaweza vikatoa bidhaa ambazo zinaweza zikawa same na zile ambazo tunataka kuzipa msamaha. Kwa maana hiyo katika miradi ile kwanza tujaribu kuangalie, kwamba Baraza la Mawaziri au N/C wajaibu kuangalia, kwamba kabla ya kukubaliana na hicho kitu kupitishwa *at least* ijulikane kwamba hicho kitu kinazalishwa nchini, kipo na kinapatikana nchini, ili *at least* kwamba na sisi viwanda vyetu viweze kufanya kazi vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kingine katika exercise duty, nazungumzia excise duty ambayo inazungumziwa katika mvinyo wa zabibu. Ninaunga mkono wazo la Serikali kuhusu excise duty kwenye mvingo, lakini tumetoa hiyo excise duty kwa ajili ya kufanya zao la zabibu pamoja na bidhaa zake zitumike. Sasa niishauri Serikali, tujaribu kutafuta matumizi, pamoja na hii ambayo ni hatua ya kikodi lakini baada ya hiyo hatua ya kikodi hebu tukaangalie quality. Wanywaji wa mvinyo wanatazama quality, kwa hiyo na sisi katika viwanda vyetu hivyo hebu tukajaribu Kwenda kufanya kitu amacho kita-improve quality. Tuki-improve quality ya wine ambayo inazalishwa ndani kwa kutumia zabibu yetu basi hapo tunaweza tukapata matumizi ya zabibu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, Serikali ijaribu kufikiria mbali zaidi kuanzisha bidhaa nyingi ambazo zitakuwa zinatumwa na zabibu au kutoa incentives katika viwanda ambavyo vitazalisha bidhaa nyingi ambazo zinatumia zabibu, hapo tutapata kuzifanya zabibu zetu kuwa zinatumika katika maeneo mengi na badala yake tutaondosha zile zabibu ambazo zipo

kwa wananchi ambazo tunasema kwamba zinaharibika. Kingine, tujaribu kukuza teknolojia juu ya utumiaji wa zabibu na bidhaa za zabibu. Pengine inawezekana teknolojia yetu ipo chini, kwa hiyo kila tunachokizalisha hapa haidhuru tutaweka *excise duty* ndogo; sasa je, kama hakuna teknolojia nzuri Je, hiki kitu kitatumika? (Makof)

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kuhusiana na suala hili, kwamba tujaribu kuwaita wawekezaji wakubwa ambao wataweza kutumia zabibu zetu ili; kwakuwa lengo ni kutaka kuwasaidia wauzaji wa zabibu; hizi zabibu ziweze kutumia lakini watengenezaji wetu wa mvinyo wa zabibu hapa huu ambao wengine wanaita mchuzi wengine wanaita togwa, utakuja kukuta kwamba wanau-store katika maeneo ambayo siyo mazuri. Kwa hiyo Serikali ijaribu ku-facilitate hili jambo ili storage katika masuala haya iweze Kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine, nitoe ushauri wa jumla. Tumesamehe baadhi ya vitu, vitu ambavyo tumesamehe ni kama vile katika mafuta. Kwenye mafuta huu msamaha ambao tutautoa kwa ajili ya wawekezaji tujaribu kuchukua hatua kuhakikisha mafuta haya ambayo yanaingizwa ndani ya nchi hii ambayo yatakuwa yamesamehewa basi *at least* yaweze kutumika kwa lengo hilo tu. Na ninaishukuru Serikali kwa hatua ambazo zipo katika mikataba ambazo zinaonesha wazi kwamba nini kitafanyika lakini tuzidi kuwa serious, kwasababu tuliwahi kuwamehe mafuta yanayokwenda kutumika migodini. Mafuta yanayokwenda kutumika migodini yalikuwa yanarudi tena. Watu wana visima vya mafuta, mafuta yale hayatumiki tena kule yanarudi mtaani yanauzwa bei ambayo siyo *fair price* ambayo biashara nyingine zinakuwa zinapata taabu. Kwa hiyo hili tujaribu kuliangalia kwa vizuri zaidi ili tuweze kulimudu na Kwenda nalo vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Naipongeza Serikali kwa kuja na mabadiliko haya. Sasa, kila tulicholenga kutoa nafuu basi kibakie palepale, kwamba kinakwenda kutoa nafuu. Tulicholenga kwenda kuzindisha uwekezaji basi kirudi pale pale na tuona kinafanya hivyo na siyo kuja kushusha biashara nyingine kwasababu ya fursa hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja kwa asilimia 100. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Daniel Parezzo, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu ajiandae ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya marekebisho ya sheria. Nitachangia katika maeneo mawili na baadaye nitatoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusiana na Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Barabara Sura Namba 220. Serikali inapendekeza hapa kutoa msamaha wa kodi katika miradi mahiri na mahiri maalum. Sasa kupitia uzoefu huko nyuma, kama ambavyo ameeleza pia Mheshimiwa aliyetoka kuongea, mara nyingi hii misamaha inaweza ikatumika vibaya kwasababu wanaofanya haya mambo sio Malaika na watu. Kwa hiyo inaweza ikawa ni kichaka cha watu kupitisha bidhaa kupata kwa unafuu na kukwepa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo amesema Mheshimiwa aliyetoka kuongea huko nyuma tulitoa misamaha kwenye miradi ya migodi watu wakawa wanapitisha mafuta yanaingia kwa mujibu wa utaratibu na ikifika migodini mafuta yanatoka yanakwenda mtaani na hivyo watu wanakwepa kodi. Kwa hiyo pamoja na mambo ambayo mmeeleza kuhimarisha mfumo wa usimamizi, kufanya ufuatiliaji na kuweka kipindi maalum ambacho kitaainishwa katika kanuni sasa haya yanayosemwa ni vema yakasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha malengo haya yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi ni lazima pia kupitia taarifa za utekelezaji ambazo zinakuja Bungeni, tuambiwe hii miradi mahiri na mahiri maalum ni ipi? Kwasababu ukiiacha tu hivyo wananchi wa kawaida wanaweza wasielewe, na hata sisi Wabunge wakati mwingine tunaweza tusiielewe; kwamba hii miradi mahiri na mahiri maalum ni ipi. Ni lazima iainishwe na tujue kwamba miradi hiyo ni ipi na itapewa misamaha na kwamba lazima kuwepo na ufuatiliaji na udhibiti ili kuhakikisha kwamba kweli mafuta hayo hayatotumika vibaya, msamaha huu uliotolewa hautatumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie pia katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 147. Serikali inaleta mapendekezo hapa ya suala la mvinyo au wine, kwamba bidhaa zinazotoka nje wanaongeza ushuru kutoka shilingi 2,466 kwa lita hadi shilingi 5,600 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa takwimu ni figure kubwa ambazo zinaongezeka; lakini sababu ya hayo marekebisho mnatuambia ni kulinda viwanda vya ndani. Sasa, kulinda viwanda vya ndani kwa bidhaa zinazotoka nje hiyo inaweza ikawa ni sababu mojawapo katika sababu nyingine nyingi. Inawezekana nyinyi mmelenga kwa mtizamo wakupata mapato halafu mkajificha kwenye kichaka cha kusema tunalinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, bidhaa zinazotoka nje kwenye huu mvinyo au wine soko la ndani bidhaa inayotoka nje ipo kwa kiwango cha asilimia 70. Nieleze hivi, bidhaa za nje, wine inayotoka nje ya nchi kwenye soko letu ipo kwa asilimia 70 wine inayozalishwa nchini kwa bidhaa za ndani ipo kwa asilimia 30. Sasa mnasema matalinda viwanda vya ndani, sawa matalinda viwanda

vya ndani, lakini kwa nini viwanda vya ndani vinaingia soko kwa asilimia 30? Hii inamaanisha kwamba kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, moja ni ubora wa wine husika. Tunapolenga kuhakikisha kwamba tunaongeza ushuru huo ili kulinda bidhaa za ndani lazima tuangalie wazalishaji wetu wakoje? Mazingira yao ya uzalishaji yakoje? Bidhaa inayozalishwa hapo inau bora? Leo hutomlazimisha mtu anunue wine kutoka ndani ilhali haina ubora akinywa labda inakereketa hapa kwenye koo au akiinunua unakuta haina ule ubora unaotakiwa. Kama lengo ni kumsaidia huyu mkulima wa mvinyo hapa nchini ni lazima kuhakikisha kuwa anatengenezewa mazingira na kumwezesha atoe bidhaa ambayo ina-quality inayoingia sokoni akihakikisha kwamba anaingia kwenye soko na anashindana.

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi lazima wajitangaze na kuhakikisha namna gani tunawasaidia kupata mitaji kama Serikali, na inawezekana hawana mitaji ya kufanya hii biashara, kwa hiyo lazima tuangalie pia kwenye suala la kuwawezesha kimitaji wafanikiwe ili nao waweze kuingia sokoni ili sasa ile asilimia 70 iwe ya ndani na asilimia 30 iwe ya nje; kwa hiyo lazima tutazame kwa mtazamo huo. Tunaposema kulinda viwanda vya ndani tuiseme kwa matendo kwa kuwasaidia. Ni vyema sana Serikali ikalitazama hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu ushauri wa jumla. Maoni ya Kamati yameeleza vizuri sana, wamependekeza kuimarisha kitengo cha utafiti wa sera za mapato, ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kitengo hiki ni lazima kiimarishe ama ki-rasilimali watu au kifedha au kiujuzi. Kwanini nasema hivi, ni kwa sababu hawa ndio ambao hatimaye kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri wanatuletea mapendeleko hapa Bungeni ya aina ya vyanzo vya mapato vinavyokuja hapa Bungeni tuvipitishe ili Serikali muweze kuenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tumeona mapendeleko ambayo yamekuja, na yako mengine ambayo leo ni kelele kwa wananchi. Kwa mfano huko nyuma kuna sintofahamu kubwa sana kwenye kodi ya majengo ambayo ilipendekezwa, kwenye tozo ya miamala ya simu na kibenki ambayo juzi umetoa kauli hapa ya kusema unaziondoa. Haya yote yanakuja na leo tunakuja kufanya marekebisho maana yake kuna tatizo mahali. Inawezekana katika kufikiria vyanzo vipi vya mapato hiki kitengo kuna shida ama ya uwezeshwaji ama upungufu wa rasilimaliwatu ama mafunzo na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, tukitaka tuone namna ya kufanikiwa katika aina ya mapato au kuwa na sera bora za mapato ambazo zitakuwa ni za uhakika na za uendelevu ni lazima tukiimarishe hiki kitengo, Kamati imeshauri vizuri sana. Kwa hiyo ni vema Serikali mkayatazama haya. Ni lazima tuwe na namna ya

kumpunguzia mwananchi mzigo. Hizo tozo zimekuwa kelele. Ndiyo, mnafanya marekebisho lakini imekuwa kelele sana lazima tufikiri hilo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine muhimu, Waziri alisema juzi hapa, kwamba wanaenda kuhakikisha wanapunguza matumizi ya Serikali. Haya yaliyosemwa ni vema sana yakaonekana kimatendo. Wakati tunapitisha bajeti hapa, Waziri alipokuwa anahitimisha alisema hivyo hivyo, lakini leo pamoja na kusema hayo kwamba tunaenda kupunguza matumizi makubwa ya Serikali bado tunayaona. Mnasema mnayapunguza lakini leo ukiona mtaani Serikali mmenunua magari mapya, new model haya ambayo yapo sokoni sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ikisema haya basi tuyaone kwa matendo. Tumetoka tu hapa kwenye bajeti tunakutana na magari mtaani. Lakini hata haya matumizi ya magari ya Serikali kwa kweli sijui tufanyeje kama Bunge, lazima yatizamwe kwa upya, magari ya Serikali baadhi, siyo yote, kwa kweli yanatumika ndiyo sivyo. Yako mengine yanapeleka maafisa na wakati huo huo wanatumia magari hayohayo kuwapeleka watoto wao shulenii, ndiyo yanayokwenda sokoni. Bosi akikaa ofisini ndiyo yanaenda kufanya kazi ya ziada. Inawapeleka watoto shule, inakwenda kuwachukua watoto shule, inakwenda sokoni. Yaani inaenda kufanya shughuli ambazo sizo. (Makof)

Mheshimiwa spika, Waziri ulisema hapa kwenye bajeti yako, tunatamani kuona utekelezaji wa kivitendo si wa kimaneno. Haya ambayo mmeyasema tuyaone kweli.

Mheshimiwa Spika, na kuna siku ulipendekeza vizuri kweli, utakuta gari linamsubiri boss linakaa masaa sita au nane liko on. Sasa hayo pia ni mionganii mwa matumizi ambayo si sahihi ya fedha za walipa kodi. Tunataka kuona mwananchi anapunguziwa mzigo wa kodi zisizokuwa za lazima na tunataka kuona matumizi ya siyokuwa ya lazima yanapungua kwa Serikali. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, sisi kama Wabunge tutaendeleza jukumu letu la kushauri na kupiga kelele. Tutapiga kelele kuhakikisha yale ambayo umeyanena tunayafulilia na tuone utekelezaji wake kwa vitendo. Ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha Namba 13 wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, nikiwa mmoja wa mjumbe wa Kamati ya Bajeti tumejadili vizuri jambo hili Muswada huu ukiwa ni Muswada muhimu kwa maudhuhi yake yote.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema lolote nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli tunaendelea kusema, Mama anasikia kwa haraka sana na anatoa maelekezo kwa haraka sana kwa ajili ya utekelezaji wa mambo mengi sana ili aweze kwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais ni kwa sababu ameona kuwa kuna kila sababu ya kurekebisha sheria kadhaa ili kuvutia wawekezaji kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na ya kielelezo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Muswada huu unakuja kuonesha ukweli juu ya Mheshimiwa Rais ambaye anaonesha kwa vitendo juu ya namna bora ya kutanzua vile vikwazo vilivyopo wakati tunatekeleza miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sehemu tano au sheria ndogo ndogo tano ambazo zipo ndani ya Muswada huu mimi nitajielekeza katika maeneo mawili. Moja ni Sheria Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147. Hapa tunarekebisha kifungu cha 128 ambacho Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Fedha anapata idhini ya Baraza la Mawaziri katika kusamehe ushuru kwenye bidhaa ambazo zitatumika kwenye miradi hii maalum na mahiri maalum. Marekebisho hayo yametusaidia kwenda kwenye hili jambo ambalo wengi wamejadili, kupandisha ushuru wa bidhaa za mvinyo kutoka takriban Shilingi 2,466 mpaka shilingi 5,600, jambo hili limekuwa ni muhimu sana. Umuhimu wake mkubwa ni kwamba unaenda kuinua kilimo chetu cha mvinyo, wengine tumesema tongwa, wengine tumezungumza lugha nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa sana ni kilimo chetu cha zabibu na vilimo vyatya aina hiyo kuweza kupata nafasi. Ni ukweli hatujafikia tu kusema 5,600 kutoka 2,466, tumeangalia kwenye nchi kadhaa za Afrika Mashariki kama comparative. Nchi nyingi zimetokea kati ya 5,000 mpaka 5,500, ambapo unaweza ukaona kwetu kwa kuwa Shilingi 2,400 na kitu ilikuwa inaweza ikasababisha hata wawekezaji wengi ambao wako hapa wakaweza kuchukua au kununua mali ghafi za mvinyo kutoka nije ya nchi. Jambo ambalo ulikuwa ni hatari sana kwa wakulima wetu na kwa muktadha mzima wa viwanda vyetu ambavyo vinachakata zao hili. Kwa hiyo, kama wazo na Kamati ilivyoshauri na kukubali mawazo ya Serikali au mapendekozero ya Serikali kwenye Muswada huu kwa kweli niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mlione hili kuwa ni jambo muhimu kwa muktadha mkubwa sana wa kuweza kuinua viwanda vyetu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini ni lazima, wengi wamesema, katika jambo hili kuna maangalizo kadhaa. Kinywaji hiki cha mvinyo ni *luxury*, wengine wanatumia kama dawa. Kwa hiyo, suala la ubora ni suala la ambalo hatuwezi ku-*compromise*, ni lazima ubora ukazingatiwe sana, hili wengi wamesema. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni uzalishaji (*production*) kwenye volumes. Kama mfano amezungumza sana Mheshimiwa aliyemaliza kusema ameweka kwenye asilimia 30 na 70. Ni hatari kama tutakuwa kama Taifa sasa bado tukawa tunazalisha chini ya asilimia 50, halafu wakati kabla hatujabadi lisha sheria hii ilikuwa tunapata kutoka nje zaidi ya asilimia 50, itakuwa ni hatari. Niombe sana Wizara ya Kilimo imepewa bajeti kubwa sana, zaidi ya mara nne katika miaka miwili hii iliyokwisha. Tangu bilioni mia mbili na hamsini na kitu mpaka bilioni mia tis ana kitu. Kwa kweli walione jicho lao likajielekeze katika eneo hili. Tunabadilisha Muswada wa sheria huu katika kifungu hiki lakini tayari fedha ziko nyingi Mama Samia kashajielekeza Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana mjielekeze kwenye kuweka mikataba ambayo hatuwezi kurudi nyuma. Tukaone ubora wa bidhaa hizi lakini vile vile tukaone uzalishaji unakuwa mkubwa ili tusiweze kuona tunadharika kutokana na mabadiliko haya ambayo tumeyadhamiria. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia nzungumzie kidogo juu ya Sheria ya Ushuru wa Mafuta wa Barabara (*The Road Fuel Tolls Act, 2022*). Hapa tunabadilisha Kifungu Namba Nane ili pia kumpa Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kusamehe ushuru wa mafuta kwa miradi ya uwekezaji mahiri na mahiri maalum. Si jambo baya, ni jambo zuri lakini tuendelee kuangalia. Uzoefu mwingi katika maeneo mengi sehemu ambayo tumepeata hasara kama Taifa ni eneo la msamaha wa mafuta, wengi wamesema migodini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini nishukuru sana Kamati ya Bajeti imeliona na imetoa mapendekezo kadhaa kwenye eneo hili. Na kubwa ni katika mapendekezo kadhaa, na ni vizuri tufahamu. Pendekozo la kwanza tumeangalia muda, pawepo na muda maalum. Tunajua miradi inaendelea kutekelezwa. Pamoja na kuangaliwa miradi hii tujue ili tukiifuatilia tunajua kabisa. Ndani ya mwaka mmoja tuweze kuangalia tumenufaika jinsi gani katika miradi hii mahiri na mahiri maalum ambayo inatekelezwa. Tukiachach wazi maana yake inawezekana miradi imekamilika halafu watu wakawa wanatupiga kupitia msahaha huu ambaa tumeuweka. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tunatambua kama nchi tunatumia mfumo mmoja wa kuagiza mafuta (*bulk procurement system*). Ni mfumo mzuri tumewahi kuujadili ndani ya Kamati vizuri kabisa, na kama nchi

tunaona bado tunafaidika na mfumo huo wa kuangiza pamoja. Sasa, inabidi tutofautishe mafuta yapi yanakuja katika mfumo huo wa pamoja na mafuta yapi ambayo yanakuja kwa ajili ya miradi maalum na mahiri maalum. Ni vizuri sana, ni muhimu. Kama tutatumia vinasaba sawa, kama tutatumia utaratibu wa uuzaji sawa, lakini ni jambo muhimu sana ili watu wasije wakapitia kwenye upenyo huo kwenda kutuumiza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeshauri pia kuweka mifumo ya usimamizi ili kuzuia matumizi mabaya ya mafuta ya miradi. Ni vizuri mifumo ikawekwa mapema, hata Mheshimiwa Waziri amesema kwenye taarifa yake, kwamba wanampango wa kufuatilia kwa karibu sana mafuta haya yanavyoingia. Mimi ninaona kwa umahiri na umakini wa Mheshimiwa Waziri kwenye jambo hili atatia nguvu sana na jicho kubwa na watalaam wake ili tusiweze kuanguka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo niseme juu ya maoni ya jumla. Kamati imeshauri sana misamaha ya kodi hii lazima iangaliwe kwa Pato la Taifa. Ndani ya mpango wetu wa miaka mitano tunaoendelea nao tumekubaliana wenyewe na tumejiwekea wenyewe kwamba misamaha ya kodi isizidi asilimia moja; hili ni jambo zuri. Sasa, Kamati inatoa ushauri kuwa wakati umefika twende tukafanye tathimini ya kina tuweze kuona mpaka sasa kwa misamaha yote ambayo imetolewa nchini imekaa vipi, ina ubora kiasi gani, tumefanikiwa au hatujafanikiwa; na kama haijazidi imezidi asilimia moja au haijazidi asilimia moja? Hili ni jambo muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niliona ni muhimu sana nichangie katika maeneo hayo mawili, na nitumie nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu waweze kuridhia Muswada huu wa Sheria Namba 13 wa Mwaka 2022 uweze kupita bila kikwazo chochote kwa maslahi mapana ya nchi yetu na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mchana wa leo na mimi kuweza kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha kwa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwasilisha marekebisho haya lakini na kwa kuwa na utaratibu wa kufanya mapitio ya sheria mbalimbali. Kwasababu sheria si msahafu wala biblia kwa hiyo kuna wakati lazima kufanya marekebisho ili kuendana na hali halisi. Kwa

hiyo, naipongeza sana Serikali kwa hatua hizi. Marekebisho haya yanalenga kuunga mkono juhudzi za mwenyewe Mheshimiwa Rais za kuhamasisha na kuvutia masuala mbalimbali ya uwekezaji. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa mashahidi wa namna ambavyo wawekezaji wengi wamekuwa wakija nchini na kujisajili katika kituo chetu cha uwekezaji. Lakini kutohana na changamoto ya utekelezaji wa Sheria ya Uwekezaji Sura ya 38 imesababisha wakati mwininge kuleta urasimu mbalimbali. Kwa hiyo kwa marekebisho haya ambayo yanaenda kurekebisha Sura ya 147 ya sheria ya ushuru wa bidhaa Kifungu 128 kumpa mamlaka Mheshimiwa Waziri baada ya idhini ya Baraza la Mawaziri nayaunga mkono kwasababu itakwenda kuondoa urasimu hasa kwenye miradi ile ya kimkakati na miradi ile ambayo mahiri. Na kwakuwa tuna matarajio ya miradi mingi nchini kwetu ikiwemo mradi wa usindikaji wa gesi asilia ninaamini marekebisho haya yamekuja kwa wakati muafaka kwa nia ya kuwezesha sasa mazungumzo yanayoendelea katika mradi huu utakapoanza rasmi. Kwa hiyo, vikwazo vilivyokuwa vinajitokeza vitakuwa havipo na mradi ambao tunautegemea kwa Taifa letu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pia imenipendeza kuunga mkono marekebiso tutakayofanya kwenye jedwali la nne kwa ajili ya kuongeza ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zinazotokana na zao la zabibu hasa huu mvinyo. Kama walivyosema wenzangu, kwamba nia hapa ni kulinda viwanda vya ndani na hii inaendana na utekelezaji wa dhima ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa ambao unasema kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa marekebiso haya ambayo yameongeza ushuru huu wa bidhaa kwa mvinyo unaoingia ndani ya nchi unawezesha viwanda vyetu vya ndani kuvilinda ambapo sasa vitatoa ajira na mwisho wa siku vitachangia kwenye Pato la Taifa kupitia kodi ambayo itakusanywa kwenye viwanda hivyo. Kwa hiyo, naunga mkono hili.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naunga mkono marekebiso yanayofanywa kwenye Sheria ya Madini Sura ya 123 (87) ambacho kinakwenda kupunguza mrahaba kwa malighafi za mbolea zinazochimbwa hapa nchini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, na jitihada hizi za kuwezesha kushushwa kwa bei ya mbolea hapa nchini napenda niipongeze sana Serikali, tumeona kwanza imetenga bilioni 150 kwaajili ya ruzuku ya mbolea; lakini kwa bajeti iliyoanza kutekelezwa tarehe 01/07/2022 tumeona hatua za kibajeti za kuweka zero rated katika malighafi zinazoingia nchini kwaajili ya kutengeneza mbolea. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zote hizi zinaainisha Serikali imeweka kwakweli mkakati makusudi wa kuinua kilimo hapa nchini, na hasa tukizingatia imeongeza bajeti zaidi ya bilioni 700 kwenye sekta ya kilimo, kilimo ambacho kitatoa malighafi kwaajili ya viwanda, kilimo kinachoajiri Watanzania wengi, kilimo ambacho kitatufanya tujitosheleze kwa chakula, lakini kilimo ambacho kitatuwezesha pia kupata mapato ambayo yatasaidia kutekeleza shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, lakini rai ambayo imetolewa na Kamati izingatiwe, kwasababu zipo hatua za kikodi zenyne nia ya kupunguza bei za bidhaa nchini lakini inapokuja kwenye suala la utekelezaji, unapokuja kwenye kufanya tathimini lile lengo la kushusha bidhaa kwaajili ya wananchi linakuwa halifikiwi. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali, kwa nia hii njema iliyokuwa nayo inabidi kwenye usimamizi iwe na ukali wa kutosha na kufanya tathimini ya mara kwa mara kwa mwenendo wa soko ili kuona kwamba ile dhamira yake inatimia. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba niunge mkono maelezo yote ambayo tumetoa kwenye Kamati na taarifa nzuri ambayo imesomwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu lakini kubwa kwenye suala zima la kuimarisha vitengo vya tafiti sera za mapato.

Mheshimiwa Spika, sisi ni Wabunge Serikali unapowasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha na vyanzo vya mapato vyenye kulenga kutatua changamoto za jamii na sisi tunatumwa kwaajili ya kuwasemea wananchi. Utakapoleta chanzo cha mapato chenye lengo la kujenga zahanati, kukamilisha maboma ya sekondari, kujenga vituo vya afya kwenye maeneo ambayo havipo, na ukizingatia takwimu zinazowasilishwa kuhusiana na changamoto hizo bado ziko kwa kiwango kikubwa, na unaiona dhamira ya Serikali ni wazi tutaunga mkono kwasababu ndilo lengo lililotuleta ndani ya Bunge. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye tathimini ya kutosha ili kuondoa mkanganyiko; kwasababu leo wanatushangaa Wabunge kwanini mnaunga mkono, lakini Serikali inafanya maboresho pia tunaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme kuwa endelea kujivunia Bunge lako, kwasababu tunapounga mkono ni kwa maslahi ya Watanzania, ni kwa maslahi ya wananchi tunaowawakilisha; na tunaiona dhamira njema ya Serikali inayoongozwa na Mama yetu. Kwa mfano hata hii hatua ya tozo tuliunga mkono kwasababu kuna dhamira ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye tarafa zote ambazo hazikuwa na vituo vya afya. Na tuliunga mkono kwasababu tuliona kwamba ni kweli zaidi ya kata 3,000 nchini hazina vituo vya afya. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uamuzi wa Serikali wa kujenga vituo vya afya ngazi ya tarafa ingetusaidia hasa akina mama ambao tunatarajia vituo vya afya. Lakini tunapokuja wakati Serikali imefanya maboresho pia lazima tuunge mkono kwasababu tunasema sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali pia kwa kusikiliza, lakini dhamira ya nia njema inabaki palepale, mchango wa kodi hiyo au tozo inabaki palepale, na historia itakuwepo. Kwamba hiyo tozo imeleta ukombozi kwasababu kwa mara ya kwanza kumejengwa vituo vya afya 234. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Bunge lako limejjengea heshima ya kukubali vyanzo hivyo; kwamba imeenda kutoa mchango sasa hivi, zahanati ni nyingi, vituo vya afya ni vingi. Pia itajenga heshima, kwamba maboresho yamefanyika na wananchi wamesikilizwa. Kwa hiyo hapa kwa lugha ya Kiswahili wanasema ni bila ni bila lakini maendeleo yameonekana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo zimewasilishwa; zina nia ya kuwezesha hivyo viwanda, lakini pia nia ya kutekeleza miradi ya kimkakati. Ninakupongeza Mheshimiwa Spika na Waziri. Tunaomba tu historia ya misamaha ambayo ilitumika vibaya isijirudie. Serikali muweke mikakati madhubuti ili misamaha itumike kwa lengo lilokusudiwa na wale watakaobainika kutumia misamaha hii kwa faida yao wachukuliwe hatua kali ikiwemo ya kulipa hiyo kodi stahiki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, utafuatiwa na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu ambaye ametuwezesha kuwepo hapa tangu asubuhi hadi sasa tukiwa katika hali ya uzima na afya pamoja na amani.

Mheshimiwa Spika, pili naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami kuwa sehemu ya wachangiaji katika hoja hii iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Waziri wangu, Waziri wa Fedha na Mipango kwa namna anavyonisaidia na kunielekeza. Lakini pili nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na makamu wake na wajumbe wote wa kamati husika nawashukuru sana kwa ushirikiano, maoni na maelekezo yao. Kwa ujumla niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao wanaotunesha ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mimi niende tu moja kwa moja katika mambo mawili ambayo kwa ujumla ni maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa

Wabunge. Maoni haya yote yapo kwa lengo la kujenga Taifa letu na kwa maslahi ya Serikali yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, maoni ambayo yametolewa na Kamati pamoja na wachingiaji moja ni usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya Serikali. Hili niseme kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango tumelipokea na tutalifanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kufanya tathmini ya kina katika misamaha yote ambayo inatolewa na Serikali kwa miradi mahiri. Nalo hili tunalichukua na tunaahidi kwamba Serikali italifanyia kazi kwa nguvu zake zote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuitemu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ili aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Na mimi nianze kwa kuwashukuru na kuwapongeza Kamati kwa maoni yao ambayo yametolewa na Mwenyekiti mahiri kabisa wa Kamati ya Bajeti, ndugu yangu Daniel Sillo. Niwashukuru pia wajumbe wa kamati, nimshukuru Naibu Waziri na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, kabla sjafafanua chochote nianze kwanza kwa kuungana na Mheshimiwa Naibu Waziri kuyapokea yale ambayo tumepewa kama ushauri. Mojawapo ikiwa ni hilo la kusimamia kwa umakini maeneo yote yale ambayo yameombewa msamaha. Niseme tu, maeneo yote yale ambayo yatapewa msamaha baada ya idhini ya Baraza la Mawaziri, misamaha hiyo itakuwa inatangazwa kwenye gazeti; na endapo itakuwa misused kama ambavyo imewekwa kwenye sheria, basi itafutwa na ikishafutwa aliyetumia vibaya atalazimika kulipa fedha hiyo ambayo itakuwa aliikoseshaa Serikali.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo linahusisha tathmini na lenyewe tumelipokea. Kimsingi tuna sura mbili kwenye masuala haya ya misamaha. Sura ya kwanza ukiangalia kwenye eneo la papo kwa papo utaona masuala yanayohusu mapato, na ukiwa hujakusanya maana yake unakuwa umekosa mapato.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa sura ya muda mrefu na matatizo ya kiuchumi kwa ujumla, utaweza kuona kwamba tunahitaji uwekezaji kwa kiwango kikubwa zaidi ili kuweza kutengeneza ajira na kuweza kutatua tatizo la ajira na kuongeza mapato katika muda mrefu, kwa maana ya

kutengeneza uwekezaji na kutengeneza fursa mpya za uzalishajji, kama ambavyo Mheshimiwa Dkt. Kimei alivyosema.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, sura hizi zote mbili ni lazima uzi-*balance*, lazima uziangalie kwa namna moja ili upande mmoja usielemewe, ukielemea upande mmoja tu wa kukusanya *in the long run* utakuwa hautengenezi maeneo mapya ya kuweza kukusanya. Kwa hiyo, hivi vyote ni vitu ambavyo vinafanyiwa *balance* na ndiyo maana unaweza ukaona kwamba maeneo yale ambayo ni ya umuhimu sana kuwekewa vivutio Serikali inaona umuhimu wa kuwekea vivutio.

Mheshimiwa Spika, jambo la tathmini na jambo la utafiti tumepokea, ni mambo ya msingi ambayo mara zote kwa ajili ya kuweza kwenda na mazingira sasa ni mambo ambavyo tunayafanyia kazi na leo tumepokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwenye eneo hili la mvinyo. Hili jambo la mvinyo tumepata fursa ya kuwasikiliza hata wakulima wenyewe. Na ukienda kwenye maeneo kwa bahati nzuri zabibu inalimwa hapahapa Dodoma kwa hiyo hatuhitaji kusafiri mbali sana kuweza kupata maoni haya.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba wakulima wetu wamebaki na mvinyo kwa kiwango kikubwa sana, na ni uhalibifu pale ambapo anakosa soko la mvinyo wake. Na kama hatua zisingechukuliwa na Serikali, ni dhahiri kwamba tunakokwenda wakulima wetu wale wangehamza kutoka kwenye kulima zabibu wangehamia labda mazao mengine, na hiyo ingeendelea kuturudisha nyuma katika hatua zetu za kulima mazao ambayo yanastawi katika maeneo husika kwa kiwango kikubwa ili tuweze kuza katika soko la ndani pamoja na soko la nje.

Mheshimiwa Spika, habari iliyojema, mara nyingi huwa tunakawaida Watanzania wakati mwingine kujikadiria kadirio la chini. Mvinyo wetu si mbaya na wala si kwamba hauna viwango vinavyotakiwa. Hivi tunavyoongea tuna mkulima mdogo tu ana kiwanda kidogo tu, lakini tayari amefikia masoko ya Zambia, Malawi, Uganda na Kenya. Kwa sasa hivi takriban kwa mwezi mmoja tuna-export zaidi ya makontena 10,000 yanakwenda China na makontena kadhaa ya mvinyo yanakwenda Italy. Sasa kama hata yanaweza kufika Italy, na China, na vilevile yameteka soko la ukanda wa kwetu hapa, nadhani si vyema kuendelea kutilia mashaka kwamba mvinyo wetu uko wa kiwango gani na uko wa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, na sasa hata vyuo vya VETA Mheshimiwa Rais alielekeza vianze kufundisha watu kazi wanazofanya katika maeneo husika. Kwa hiyo, tutaendelea hata kuboresha zaidi kuweza kuyafikia na masoko mengine.

Mheshimiwa Spika, na la mwisho Mheshimiwa Cecilia nilimsikia akisema kwamba yasiwe maneno tu iwe vitendo. Moja ya wakati ambapo tunaishara nyingi sana za vitu vinavyofanyika kuliko maneno nadhani ni wakati huu. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha mwaka mmoja tu vitu ambavyo amevifanya vingekuwa vinapigiwa kelele nadhani vingekuwa vimevuta mipaka hata ya nchi yetu yenye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mimi ningearabiwa nimuelezee Rais Samia Suluhu Hassan kwa sentensi moja, kitu kimoja tu ambacho ningesema, sentensi hiyo ingekuwa nchi inasonga mbele kwa kasi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo si maneno ni vitendo. Yaani tunavyosema nchi inasonga hakuna mradi mmoja wowote mkubwa umesimama hata kwa wiki moja tu. Miradi yote mikubwa inaendelea. Lakini na nyongeza, katika kipindi cha mwaka mmoja tu, na ninyi ni Wabunge ndio wawakilishi, wa wananchi; barabara zimejengwa vijiji kuliko mwaka wowote ule katika record tangu uhuru. Tuna vijiji ambavyo tangu uhuru havikuwahi kupata barabara, lakini barabara hizo zimejengwa katika kipindi cha mwaka mmoja na zinapitika. Kwa hiyo, si maneno, ni vitu ambavyo wananchi wanaviona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, tuna taraja ambazo hazikuwahi kuwa na vituo. Katika kipindi cha mwaka mmoja zimepata vituo na sasa hivi hatua inayofuata ni kwenda kuviwekea miundombinu ama vifaa tiba ili viweze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si hayo tu, hata hii tuliyosema juzi kwamba tutabana matumizi si maneno ni jambo ambalo tunaenda kufanya. Tunamaliza makusanyo ndani ya mwisho wa mwezi huu, wiki ijayo tutaoa bilioni 160 kwaajili ya kupeleka ujenzi wa madarasa ambayo Mheshimiwa Rais amesema ifikapo Januari pasiwe na second selection. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana hapakuwa na second selection kwa vitendo watoto wote walienda shulen shule zilipofunguliwa. Na mwaka huu Rais ameelekeza ifikapo Januari madarasa hayo yawe yameshajengwa, hapatakuwa na second selection. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeshaongea na Mheshimiwa Bashungwa, Waziri wa kisekta, wiki ijayo shughuli hiyo inaanza na fedha hizo sehemu zitakuwa zimetoka kwenye makusanyo, sehemu zinatoka kwenye kukata matumizi kufidia sehemu ile ambayo tumeisema katika kauli yetu. Kwa maana hiyo si maneno ni vitendo na vitendo hivyo vinaonekana na vinaongea kwa sauti kubwa kuliko maneno.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufuatiliaji tutashirikiana na wenzetu wa mamlaka ya mapato pamoja na Wizara zingine za kisekta ili kuweza

kuhakikisha tunafuutilia. Hata jana tulipokuwa kwenye Kamati tulikuwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na sekta zingine.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ambayo yatahitaji performance agreement tutafanya hivyo ili kuweza kufanya ufuutiliaji unaopimika, na haya tayari tumeshaanza katika sekta zingine ambako maeneo yale tuliweza kuahidi hapa katika Bunge lako Tukufu wakati wa Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimeyasema hayo, nirejee tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na naomba sasa kutoa hoja. (Makofii)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na sasa tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge Zima.

**SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima.

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 (The Written Laws Financial Provisions Amendments Bill, 2022)**

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 4

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 5  
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**22 SEPTEMBA, 2022**

(Bunge Lilirejea)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 (*The Written Laws Financial Provisions Amendment Act, 2022*) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. Taarifa hiyo sasa ikubaliwe na Bunge rasmi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha zipatazo sita kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo (*A bill for an Act to Amend Certainly Written Laws in order to keep the laws updated with some challenges observed in its implementation*).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu na sisi tumemaliza kwa hatua yetu. Sasa niwahoji, naona hapa nilipaswa kuwahoji kabla ya kusomwa kwa mara ya tatu.

Waheshimiwa Wabunge sasa niwahoji, Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 yaani *The Written Laws Financial Provisions Amendments Bill, 2022*, waseme ndiyo.

(Hoja llitolewa lamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Hakuna ambao hawajaafiki, wote wameafiki sheria hii kupidishwa na Bunge na sasa nimpe fursa Katibu ya kusoma kwa mara ya tatu. (Makofi)

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha zipatazo sita kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo (A bill for an Act to Amend Certainly Written Laws in order to keep the laws updated with some challenges observed in its implementation) Ulipitishwa na Bunge.**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu na sasa sisi kwa sehemu yetu tumeshamaliza zoezi la kutunga sheria. Na kwa Muswada huu ulivyokuwa tulikuwa tunabadilisha baadhi ya sheria, vifungu ambavyo vilikuwa vinaleta changamoto kwenye utekelezaji ambavyo pengine kwa namna moja au nyingine vilikuwa vinaleta changamoto kwenye uwekezaji na vingine kwenye mambo mengine kama kuwasaidia wakulima hasa kwenye eneo hili la zabibu.

Kwa hiyo, kwa sehemu yetu sisi tumemaliza kazi na sasa tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye afanye kwa sehemu yake kwa kadri anavyohitajika kufanya hivyo na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka yeye asaini halafu akishasaini basi tutakuwa tumeshapata sheria iliyokamili.

Kwa hivyo, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuyaona haya mapungufu ambayo mengine yametokana na michango ya Wabunge. Kwa hiyo, ninawapongeza sana kwa hatua mlizozichukua ili kuleta marekebisho haya na Bunge kuweza kuchukua hatua zile ambazo zinastahiki.

Lakini niishukuru pia Kamati yetu ya Bajeti kwa kazi nzuri walioifanya ya kutumia muda mfupi ambao walipewa, wameweza kufanya kazi hii vizuri na sisi wote ni mashahidi kwa mapendekezo ambayo waliyatoa wakajadiliana na Serikali na Serikali ikayakubali pamoja na kwamba muda ulikuwa mfupi. (Makofi)

Kwa hiyo, tunawapongeza sana Kamati yetu ya Bajeti na Wabunge wote kwa ujumla ambao mmeshiriki kwenye zoezi hili. Wengine si wajumbe wa Kamati ya Bajeti lakini mmepata fursa ya kuchangia humu. Na kama Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri walivyosema, kwamba mawazo yenu ameyachukua hata yale ambayo hayakuwa yanahu moja kwa moja utungaji wa sheria, na wataendelea kuyafanyia kazi. Na mengine yale ambayo watahitaji kuyatumia katika utekelezaji wa haya mabadiliko, basi watafanya hivyo. Na sisi tunawatachia kila la kheri katika hayo. (Makofi)

Ni muhimu sana, hasa katika lile eneo ambalo Wabunge wamesisitiza kuhusu hii misamaha itakayokuwa inatolewa kuendelea kufuatilia ili isilete changamoto ambazo ziliwahi kujitokeza huko nyuma. Hilo ni la kwanza. Jambo la pili ni kuhusu huu mchuzi wa zabibu tunaosema mchuzi sijui togwa ya zabibu, lakini ni muhimu viwanda vyetu viwe na huo mchuzi wa kutosha. Maana isije kuwa tumezuiwa kuingia halafu kilimo cha zabibu kikaanza kusuasua; na sasa hivi kilimo wameshongezewa pesa nyingi na Mheshimiwa Rais kwenye bajeti yao, ililetwa na Bunge likapitisha.

Kwa hiyo tunaamini mtakuwa mmeweka mazingira ambayo huu mchuzi utatosheleza viwanda vyetu hapa ndani na usitengeneza mazingira ambayo sasa viwanda vitakuwa vinahitaji mchuzi halafu hapa sheria tumeshabadilisha, halafu hayo matokeo yake yanazifanya bidhaa tena ziende juu kwa sababu bidhaa itakuwa ni adimu.

Kwa hiyo tunawatachia kila la heri katika kuhakikisha sekta hizi zinafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha mambo yanaenda vizuri na Wabunge wamefanya kwa sehemu yao kwa uhaminifu kabisa ili kuwapa ninyi vitendea kazi ama nyenzo na tuna amini mtazitumia vizuri ili tuendelee kuisaidia nchi yetu isonge mbele.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa ratiba yetu ile; kabla hatujaenda kwenye Miswada ya Sheria ya Serikali kuna ratiba tulikuwa hatujaikamilisha pale juu sasa ndio wakati wa kuikamilisha. Kwa hivyo tumwite katibu atusomee matokea ya uchaguzi.

#### **MATOKEO YA UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba tuanze na Kundi A - Wagombea Wanawake, kura zilizopigwa ni 322 matokeo ni kama ifuatavyo:-

Ndg. Angela Charles Kizigha	kura 322,
Ndg. Nadra Juma Mohamed	kura 310,
Dkt. Shogo Richard Mlozi	kura 322,
Ndg. Zainab Ham Abdul	kura 1,
Ndg. Queen Julieth Lugembe	kura 9, na
Ndg. Sonia Jumaa Magogo	kura 2.

Mheshimiwa Spika, Kundi B - Wagombea wa Zanzibar, idadi ya kura ni 322, kura zilizoharibika ni 11, matokeo ni kama ifuatavyo:-

Dkt. Abdulla Hasnuu Makame	kura 305,
Ndg. Machano Ali Machano	kura 291,
Ndg. Husna Mohamed Abdalla	kura 4,

Mhandisi Mohamed Habibu Myaa kura 7, na  
Ndg Anderson Ndambo kura 2.

Mheshimiwa Spika, Kundi C Wagombea wa Vyama vya Walio Wachache Bungeni, idadi ya kura zilizopigwa ni 320 na kura moja imeharibika. Matokea ni kama ifuatavyo:-

Ndg. Ado Shaibu Ado	kura 78,
Ndg. Jafar Said Mneke	kura 7, na
Ndg. Mashaka Khalfan Ngole	kura 234.

Mheshimiwa Spika, Kundi D - Wagombea wa Tanzania Bara, kura zilizopigwa ni 322, kura tisa zimeharibika. Matokeo ni kama ifuatavyo:-

Ndg. Ansar Abubakar Kachwamba	kura 300,
Ndg. James Kinyasi Millya	kura 312,
Dkt. Ng'waru Jumanne Maghembe	kura 311,
Ndg. Adui Seif Kondo	kura 10,
Ndg. Mohamed Msham Ngulangwa	kura 3, na
Ndg. Thomas D. C. Malima	kura 3.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, timesomewa matokeo ya kura na sasa ni kazi yangu kuwatangaza washindi kwenu kwa mujibu wa kura hizi zilizosomwa na katibu. Tulikuwa tunahitaji kuchagua Wabunge tisa kwa ajili ya kwenda kutuwakilisha na mimi nitawatangaza hao tisa ambao wameshinda kwa mujibu wa kura zilizosomwa na msimamizi wa uchaguzi.

Wa kwanza ni Ndugu Angela Charles Kizigha, sasa hii sio kwa idadi kura hawa wanasmwa kwa kadri walivyoandikwa hapa mbele Ndugu Nadra Jumaa Mohamed, wa tatu ni ndugu huyu ni daktari jamani Dkt. Shogo Richard Mlozi, wanne ni Dkt. Abdulla Hasnuu Makame, wa tano ni Ndugu Machano Ali Machano, wa sita ni Ndugu Mashaka Khalfan Ngole wa saba ni Ndugu Ansar Abubakar Kachwamba, wa nane ni Ndugu James Kinyasi Millya wa tisa ni Dkt. Ng'waru Jumanne Maghembe. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuwapongeza sana hawa ndugu zetu kama ingekuwa katika utaratibu ule wetu wa kawaida na zoezi kama lisingechukuwa muda mrefu kwa sababu wakishachaguliwa namna hii awapati tena fursa ya kuingia humu ndani, na ni siku ya leo tu ndiyo tumetengua kanuni ili wao waruhusiwa kuingia humu ndani. Kwa hiyo kama tungekuwa hatujakaa muda mrefu sana ningewapa fursa ya kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kura mlizowapa.

Hata hivyo sitawaruhusu kuzungumza nanyi lakini nitawaruhusu wote kwa pamoja waingine humu ndani watatoa ishara ya shukrani kwenu Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Kwa hiyo wale Wabunge sasa ambao tumeshawachagua wanaosubiri kuapa wanaruhusiwa sasa kuingia humu ndani ili watoe shukrani zao na watatoa kwa ishara badala ya kuzungumza.

*(Hapa Wabunge Wateule wa Bunge la Jumuia ya Afrika Mashariki waliingga ukumbini)*

**SPIKA:** Ndugu Angela Charles Kizigha, Ndugu Nadra Jumaa Mohamed, Dkt. Shogo Richard Mlozi, Dkt. Abdulla Hasnuu Makame, Ndugu Machano Ali Machano, Ndugu Mashaka Khalfan Ngole, Ndugu Ansar Aboubakar Kachwamba, Ndugu James Kinyasi Millya ana Dkt. Ng'waru Jumanne Maghembe.

Haya waendelee kuingia kwa kadri ya majina yao Ndugu Angela Charles Kizigha wote mnaingia kwa pamoja anafuatiwa na Ndugu Nadra Jumaa Mohamed kama alikuwepo bado, halafu Dkt. Shogo Richard Mlozi, haya Dkt. Abdulla Hasnuu Makame, Ndugu Machano Ali Machano, sogeeni tu mbele Ndugu Mashaka Khalfan Ngole, Ndugu Ansar Aboubakar Kachwamba haya Ndugu James Kinyasi Millya Ndugu Ng'waru Maghembe Jumanne. Haya hao hao waliongozana haya wakishafika hapa mbele karibuni sana.

Wabunge tisa ambao wamechaguliwa kwenda kuiwakilisha nchi yetu ni hawa hapa mbele yenu, na sasa hili muweze kuwakumbuka kwa majina na sura atakayekuwa ametajwa msogee nyuma nyuma kidogo msogee upande ule haya atakayetajwa anapita mbele anainama anawageukia Wabunge anarudi nyuma.

*(Hapa kila Mbunge Mteule wa Bunge la Jumuia ya Afrika Mashariki aliinama ikiwa ni ishara ya kushukuru baada ya kuitwa jina na Spika)*

**SPIKA:** Ndugu Angela Charles Kizigha, Waheshimiwa Wabunge Mbunge wenu huyo mmemchagua kwa niaba ya nchi nzima; Ndugu Nadra Jumaa Mohamed, haya Waheshimiwa Wabunge mwakilishi wetu huyo; Dkt. Shogo Richard Mlozi, haya ahsante sana mwakilishi wetu huyo; Ndugu Dkt. Abdulla Hasnuu Makame mwakilishi wetu mwingine huyo; Ndugu Machano Ali Machano, ahsante sana, Ndugu Mashaka Khalfan Ngole, mwakilishi mwingine huyo; Ndugu Ansar Aboubakar Kachwamba, ahsante sana mwakilishi wetu huyo mwingine; Ndugu James Kinyasi Millya mjumbe wetu mwingine huyo na Dkt. Ng'waru Jumanne Magembe. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo Wabunge ambao tumewachagua sisi siku ya leo kwa niaba ya wananchi wote kwenda

kutuwakilisha kama Tanzania kwenye Bunge la Afrika Mashariki, na tunawategemea mnapoenda kule si hoja ya mawazo yenu ni hoja ya nchi inasemaje. Tunaamini mtaenda kusimamia maslahi ya nchi kama mlivyoahidi hapa. Sisi humu ndani tumewachagua kwa niaba ya Watanzania wote, mnakwenda kuwakilisha Watanzania wote pamoja na kwamba sisi ndio tumewachagua.

Jambo lingine ni umuhimu wa kuzingatia kazi zile ambazo mnapaswa kuzifanya huko, huku lazima mtuletee taarifa za kazi zenu kwa kadri ambavyo mnatakiwa kufanya hivyo na kanuni.

Lingine kulikuwa na maswali hapa na pale, niwape tu ushauri kama ambavyo sisi huwa tunaenda majimboni kwetu ninyi jimbo lenu ni hili hapa kwa niaba ya Tanzania nzima. Kwa hiyo Wabunge wote hawa, mimi ninazungumzia kwa niaba yao, wanawatachia utumishi mwema, na wanaamini mtaenda kufanya vizuri na hamtaenda kufanya tofauti; kila la kheri. Ahsanteni sana. Sasa mnaweza kwenda. (*Makofii*)

(*Hapa Wabunge Wateule wa Bunge la Afrika Mashariki waliondoka ukumbini*)

**SPIKA:** Sasa leo Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mnashangaa kidogo, ni kwa sababu kanuni zimetenguliwa, kwa hiyo ndio maana na mimi nimesimama na wengine wanasimama, kwa hiyo msiwe na wasiwasi leo kanuni zimetenguliwa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu bado nimesimama hapa nipeni muda nimalize halafu tukwapongeze hapo nje kidogo. Waheshimiwa Wabunge, naona mnawakaribisha na kwenye viti kabisa; haya ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana kwa uvumilivu wenu, kwa siku ya leo maana kulikuwa hakuna mapumziko na tumeanza kazi tangu asubuhi na tunamaliza muda huu. Nina washukuru sana kwa uvumilivu wenu wa kufanya kazi hii kuwa lazima ikamilike ahsanteni sana.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahilisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 9.56 alasiri Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,  
Tarehe 23 Septemba 2022 Saa Tatu Asubuhi*)

**22 SEPTEMBER, 2022**